

MAUDHUI YA UKUNGWI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB

FADHILI HAMISI WENDO

C50/OL/MSA/20611/2022

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA
KENYATTA**

NOVEMBA , 2025

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Sahihi: _____

Tarehe: 18/11/2025

Fadhili Hamisi Wendo

C50/OL/MSA/20611/2022

Tasnifu hii limetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi: _____

Tarehe: 10/11/2025

Dkt. Titus Kaui

Idara Ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta



TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi hususan mamangu Fatuma Hamisi Wendo na marehemu babangu Hamisi Abdallah Wendo kwa kunipenda kwa dhati, kunisomesha na kuniombea kwa Mola kila kukicha.

SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa kuniongoza kila uchao. Toka nilipojitosa ndani ya bahari hii ya masomo, mambo mbalimbali yalikwenda segemnege ila Mungu alinishika mkono hadi kufikia tamati.

Vilevile, ningependa kuwapa shukrani zangu kutoka kwenye moyo wangu kwa dua njema mlizokuwa mkiniombea kila wakati na Mungu atawalipa maradufu. Natoa shukrani kwa ndugu zangu Mohammed, Omar, Hanifa, Bebi, Mwatime na Abdalla kwa kunisaidia katika hali tofauti.

Aidha, namkabidhi shukrani za dhati msimamizi wangu Dkt. Titus Kau. Umejizatiti kwa kunielekeza, kunishauri na kuipiga msasa kazi hii kwa uwezo wako wa kupigiwa mfano. Nakuombea maisha mema yanye furaha na baraka. Shukrani za dhati pia ziwafikie wahadhiri wangu walionijaza maarifa; Prof. Wafula, Prof. King'ei, Prof. Chacha, Prof. Pamela, Pof. Githinji, Dkt. Masinde, Dkt. Nandama, Dkt. Kamau, Dkt. Murithi, Dkt. Bethi, Dkt. Mburu, Dkt. Kihara, Dkt. Osore, Dkt. Boniface, Dkt. Arege, Mwal. Mudhune na Mwal. Mukobwa. Maarifa mlonijaza sina cha kuwalipa ila kuwaombea dua kwa Rahman kuwajaza elimu na maarifa zaidi.

Tamati, shukran za dhati ziwaendee wanafunzi wenzangu; Wilson, kwa hakika umenifaa sana, Maggret, Hawa na Nikodemus kwa umoja wenu mlionionyesha na kunitia motisha kwa ushauri mwema. Ningependa pia, kuwashukuru wandani wangu wa karibu; Hamisi Mwanyumba, kwa kweli umenifariji sana, Salim Ganyuma, Yussuf Njia, Abdalla Sarai, Summayah, Fatuma Bakari, Tatu Bya, Omar Rajab na Edwin kwa kweli mumenisaidia sana. Sina cha kuwalipa zaidi ya kuwaombea mema kwa Mungu.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
YALIYOMO.....	v
UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU	ix
IKISIRI	x
ABSTRACT.....	xi
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI.....	1
1.0 Usuli wa Mada	1
1.1 Suala la Utafiti.....	6
1.2 Malengo ya Utafiti	6
1.3 Maswali ya Utafiti.....	7
1.4 Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada	8
1.6 Upeo na Mipaka	9
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada.....	10
1.8 Msingi wa Nadharia	13
1.8.1 Nadharia ya Simiotiki.....	13
1.8.2 Nadharia ya Uamilifu	14
1.9 Mbinu za Utafiti	15

1.9.1 Eneo la Utafiti	15
1.9.2 Uteuzi wa Sampuli	16
1.9.3 Ukusanyaji wa Data	16
1.9.4 Uchanganuzi wa Data.....	17
1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo	18
1.10 Maadili ya Utafiti	19
SURA YA PILI.....	20
DHIMA YA KUNGWI KATIKA JAMII YA WASWAHILI	20
2.0 Utangulizi	20
2.1 Historia Fupi ya Utamaduni wa Waswahili	21
2.2 Dhima ya Kungwi katika Jamii ya Waswahili	24
2.2.1 Namna ya Kumhudumia Mume	25
2.2.2 Mafunzo ya Vifaa na Maana yake.....	29
2.2.3 Namna ya Mke Kuhusiana na Watu Wengine	36
2.2.4 Namna ya Kuzungumza na Mume	38
2.2.5 Uzingativu wa Usafi.....	39
2.2.6 Adhabu kwa Wanawali Wasiotii	41
2.3 Hitimisho	42
SURA YA TATU.....	43
MAUDHUI YA UKUNGWI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB	43
3.0 Utangulizi	43
3.1 Asili ya Nyimbo za Taarab.....	43
3.2 Maudhui ya Ukungwi katika Nyimbo Teule za Taarab	45

3.3 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa <i>Maji ya Uvuguvugu</i> wa Wachonga Vinyago	46
3.4 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa <i>Bi. Arusi</i> wa AT	50
3.5 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa <i>Ndoa</i> wa Aslay na Hadija Kopa.....	54
3.6 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa <i>Nenda Salama</i> wa Omari Kopa	58
3.7 Hitimisho	63
SURA YA NNE	64
MWINGILIANO KATI YA DHIMA YA KUNGWI KATIKA JAMII NA MAUDHUI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB	64
4.0 Utangulizi	64
4.1 Mwingiliano wa Tanzu na Vitanzu vya Fasihi.....	64
4.2 Mwingiliano kati ya Dhima ya Kungwi katika Jamii na Maudhui katika Nyimbo teule za Taarab.	67
4.2.1 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui ya Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Uhusiano wa Mke na Mumewe	69
4.2.2 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui katika Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Uhusiano kati ya Mke na Jamaa za Mumewe	74
4.2.3 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui katika Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Kujitunza kwa Mke.	76
4.3 Hitimisho	78
SURA YA TANO	79
MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO	79
5.0 Utangulizi	79

5.1 Muhtasari wa Utafiti.....	79
5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo	81
5.3 Mchango wa Utafiti.....	85
5.4 Changamoto za Utafiti	86
5.5 Mapendekezo ya Utafiti	87
MAREJELEO	89
VIAMBATISHO	93
KIAMBATISHO A: NYIMBO TEULE ZA TAARAB.....	93
KIAMBATISHO B: KIELELEZO CHA HOJAJI KWA MAKUNGWI LENGWA. 102	
KIAMBATISHO B: VIBALI VYA UTAFITI	103

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

- Kungwi:** Ni mtu ambaye humfundisha mwanamwali wa kike au wa kiume kunga za nyumbani au masuala ya unyumba.
- Mitishamba:** Dawa za kiasili
- Taarab:** Ni nyimbo zenye asili ya Kiarabu zinazoimbwa katika Pwani ya Afrika Mashariki ambazo hutungwa kwa kutumia lugha ya kimafumbo, yenye mvuto na mnato.
- Unyago:** Ni mchakato wa kuingiza mtu katika hatua mpya ya maisha yake huku akipokezwa mafunzo maalum ya jamii yake.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza jinsi maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab. Malengo yafuatayo yalinuiwa kutekelezwa; kubainisha dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili, kuchunguza maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab na kulinganisha dhima ya kungwi na maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Sampuli iliteuliwa kimaksudi ambapo kati ya nyimbo nyingi za taarab, nne ndizo ziliteuliwa kutumika katika utafiti huu. Nyimbo hizi ni: *Maji ya Uvuguvugu* (Wachonga Vinyago), *Nenda salama* (Omar Kopa), *Ndoa* (Aslay na Khadija Kopa), *Bi Harusi* (AT). Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya kimakusudi. Kati ya maeneo mengi katika jamii ya Waswahili, eneo la Msambweni ndilo lililoteuliwa kutumika katika utafiti. Mbinu hii ilifaa katika kuwateua makungwi waliochangia data muhimu ya kuchanganuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Uamilifu. Nadharia ya Simiotiki iliasisiwa na Ferdinand Dessaussure (1913) na Charles Pierce (1977) na inahusu uhusiano uliopo kati ya kitaja na kitajwa na matumizi ya ishara, picha na msimbo. Nadharia hii ilisaidia katika kufafanua mbinu za uwasilishaji wa ujumbe katika nyimbo teule za taarab. Kwa upande mwingine nadharia ya Uamilifu iliasisiwa na Emile Dukheim (1912) na inahusika na uchambuzi wa dhima zinazojitokeza katika kazi za fasihi. Hii ilituongoza katika kubainisha dhima ya kungwi katika jamii. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktaba na wa nyanjani ambapo maktabani; mtafiti aliweza kusoma tasnifu, makala na majarida yanayohusiana na mada. Nyanjani, mtafiti alitembelea eneo lengwa ili kuwahoji baadhi ya makungwi kuhusu dhima yao. Matokeo yalionyesha kuwa kungwi ana jukumu la kuwafundisha wanawali kuhusu maswala ya unyumba yakiwemo usafi wa mwili na nyumba, namna ya kumhudumia mume, namna ya kusema na marafiki na jamaa za mume, matumizi ya vifaa vya kiasili kama vile mbuzi, kinu, mchi ufagio miongoni mwa mengine. Aidha, maudhui haya ya ukungwi yanafundishwa na waimbaji wa nyimbo teule za taarab na kuonyesha namna kipera cha nyimbo na mawaidha vinaingiliana kimaudhui. Utafiti huu unatarajiwa kutoa mchango wa kuonyesha jinsi vitanzu vya mawaidha na nyimbo huingiliana kidhima.

ABSTRACT

This study analysed the role of a *Kungwi* (lose translation of the term) and how it is depicted in selected taarab songs. A *Kungwi* is a person who teaches a female or a male adolescent about marriage and its responsibilities. The following objectives were intended to be achieved; to determine the role of a *Kungwi* in the Swahili community, to analyse the theme of marriage education in the selected taarab songs, and to compare the role of a *Kungwi* and the the theme of marriage education in the selected taarab songs. The study sample was purposively selected where among many taarab songs, four were selected to be used in this study; *Maji ya Uvuguvugu* (Wachonga Vinyago), *Nenda salama* (Omar Kopa), *Ndoa* (Aslay na Khadija Kopa) and *Bi Harusi* (AT). Msambweni area of the coastal region of Kenya was selected purposively as the study area. The research was guided by two theories: Semiotics and Functionalism. Semiotics was invented by Ferdinand Dassaussure (1913) and Charles Pierce (1977). It explains the relationship between the reference and the referent and the use of symbols, images and codes. This helped in clarifying the themes of marriage education in the selected taarab songs. On the other hand, Functionalism theory was invented by Emile Dukheim (1912) and it deals with the analysis of the role of literary works. This guided us in determining the role of a *Kungwi* in the Swahili community. This research was library and field centered where in the library, the researcher was responsible for reading dissertations, articles and journals related to the topic. In field, the researcher visited the study area to interview some *Kungwi* about their role. The research found out that, a kungwi has a role of teaching the adolescents their role in marriage which includes; maintaining cleanliness of both the body and the house, how to relate with people, how to treat a husband, how to use idigeneous items like, a broom and many others. In addition, the research found out that these roles are also taught by selected taarab singers depicting a relationship between genres of oral literature. This research is expected to give an understanding of the similarities in the roles of some genres of oral literature.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada

Kungwi ni mtu anayefundisha mwanamwali wa kike au wa kiume kunga za nyumbani (Ngwabi, 2020). Kungwi pia huitwa somo. Makungwi hupatikana katika jamii ya Waswahili ambapo huwafunza wanawali kuhusu mambo mbalimbali ya unyumba. Kiriimi (2014) anaeleza kuwa katika sherehe za unyago ndipo makungwi au somo huchukua kujukumu la kuwafundisha wanawali wa kike. Japo watoto wa kiume hupata mafunzo katika sherehe za jando, uzingativu mwingi huwa kwa wanawali wa kike. Katika jamii ya Waswahili, mafunzo ya unyago huanza pindi tu mtoto wa kike anapoanza kupata hedhi. Mafunzo haya hufanywa na kungwi.

Kwa mujibu wa Kiriimi (keshatajwa), kungwi anapaswa kuwa mwanamke ambaye ameolewa na aliye na ufahamu kuhusu desturi za jamii. Anaweza kuwa shangazi wa mwanamwali au rafiki wa karibu wa mama wa mwanamwali. Kungwi ana majukumu mengi yakiwemo kuwafundisha wanawali kuhusu namna ya kuwatunza wanaume wao, upishi, desturi za jamii, namna ya kupamba nyumba na miili yao kwa manukato, namna ya kujitunza wakati wa hedhi miongoni mwa dhima nyingine. Saumu (2011) anaeleza kuwa mafunzo haya huanza punde tu baada ya mwanamwali kuanza kupata hedhi. Anaendelea kueleza kuwa, mafunzo haya ya kwanza yanafahamika kama dari ya mwanamwali. Opweho (1992) anaeleza kwamba ni katika kipindi hiki cha kuanza

kupata hedhi ndipo wanawali wa kike wanatengwa na kupokea mafunzo. Kungwi vilevile analo jukumu la kuwaadhibu wanawali wanapokosea katika mafunzo hayo.

Kando na hayo, Kirimi (keshatajwa) anaeleza kuwa makungwi wana dhima nyingine ya ‘kuthibitisha ubikira’ wa wanawali wakati wa mafunzo ya unyago. Katika jamii ya Waswahili, ubikira wa wanawali wa kike unathaminiwa sana kabla ya ndoa yao. Ili kufanikiwa katika uthibitishaji wa ubikira wa mwanamwali, kungwi huunda uhusiano mwema baina yake na mwanamwali anayemfundisha. Baada ya hili, humuuliza maswali ya moja kwa moja iwapo amewahi kushiriki tendo la ngono. Mbinu nyingine anayotumia ni kumshawishi mwanamwali kwa visa vya kubuni kuhusiana na ngono vinavyolenga kumchochea kufichua ukweli kuhusu iwapo ameshavunja ubikira wake au la. Iwapo itabainika kuwa mwanamwali ameshapoteza ubikira wake basi kungwi wake atampa mitishamba ili kumrejeshea ‘ubikira’ wake na hili linabaki kuwa siri kubwa baina yao. Ijapokuwa uthibitishaji wa ubikira wa mwanamwali katika jamii ya Waswahili hufanyika siku ya ndoa wakati wa tendo la ngono, kungwi hutekeleza jukumu hili kabla ya ndoa. Lengo kuu la kungwi kufanya hivi ni kudumisha hadhi ya mwanamwali pamoja na familia yake siku ya ndoa wakati wa ‘ushuhuda wa damu’.

Fair (1996) anaeleza kuwa Waswahili asilia wa pwani ya Afrika Mashariki hawakuwa na utamaduni huu wa mafunzo ya unyagoni bali waliuiga kutoka kwa jamii zengine za Kiaribu. Kutokana na utumwa, sherehe za unyago zilikita mizizi katika jamii ya Waswahili karne ya kumi na tisa. Strobel (1984) anabainisha kuwa majukumu ya wanawake katika ndoa yanayofundishwa na makungwi yalianza zamani karne ya kumi

na nane. *Utenzi wa Mwanakupona* uliotungwa kabla ya karne ya kumi na nane ambao umesheheni mafunzo ya unyumba kwa wanawake kwa misingi ya dini ya Kiislamu. Jamii ya Waswahili hutumia utendi huu kama msingi wa maadili ya ndoa kwa mwanamke. Wakati wa mafunzo kwa mwanamwali yanayofanywa na kungwi, utendi huu vile vile hurejelewa mara kwa mara. Mawaidha na mafunzo ambayo makungwi huwapa wanawali huhusisha masuala ya utiifu kwa mume na namna ya kumshughulikia mume (Trimigham 1980).

Kadri muda unavyozidi kusonga dhima hii ya makungwi imeanza kutekelezwa na baadhi ya wasanii katika nyimbo zao teule za taarab. Dhana ya taarab imeweza kufasiriwa na wataalam mbalimbali, Makila (2011) anafafanua kuwa taarab ni muziki au nyimbo ambazo hutungwa kutumia lugha ya kimafumbo, yenye mvuto na mnato. Anazidi kueleza kuwa muziki huu unapochezwa hauzui familia yaani baba, mama na watoto kusikiliza au kutazama wakiwa pamoja.

Kulingana na Makilla, taarab asilia ni muziki wa kutazama, kusikiliza, kutunza na kutafakari bali si muziki wa kucheza. Khamis (2005) naye anaeleza kuwa taarab ni neno lenye asili ya Kiarabu lilitokana na neno ‘tariba’ lenye maana kujitikisa, kufurahi, kuimba na kupiga muziki kwa ajili ya kucheza na kujifuraisha. Hivyo basi taarab ni muziki unaoleta furaha na kuondoa mawazo ili kuibua hisia zenye raha, anasa na huambatana na maneno ya kishairi, ambayo yanatumia ala za muziki (Rajab 2016) taarab inaambatana na ala za muziki kama vile dumbaki, ganuni, filda, kinanda na dabalibesi. Kwa ujumla

basi nyimbo za taarab ni aina ya nyimbo zinazotumia lugha ya kimaumbo na zenye kuibua hisia mbalimbali za furaha, msimsimko na mapenzi ambayo hutazamwa au kusikilizwa.

Nyimbo za taarab ni nyimbo zenye historia ndefu tangu miaka ya 1870 katika visiwa vya Zanzibari kutokea nchi za uarabuni. Taarab asilia iliimbwa katika nyimbo ya Kiarabu kwa kuwa ilidhamiria kuwastarehesha watawala ambao wengi wao walikuwa wenye asili ya Kiarabu. Kuanzia miaka ya 1990 nyimbo za taarab zilianza kuimbwa katika lugha ya Kiswahili jambo ambalo lilipelekea taarab asilia kueleweka na kuvutia zaidi. Jambo hili lilipelekea baadhi ya wataalam kudai kuwa asili ya taarab ni Uswahilini na chimbuko lake ni Zanzibar (Abdalla, 2018).

Fair (2001) anasema kwamba, mwanamuziki wa kwanza kusifika wa taarab ni Siti Binti Saad kutoka Zanzibar, mwanamke mwenye asili ya Uafrika. Alisifika kwa kipaji chake kikubwa katika uimbaji wa muziki wa taarab na sauti nzuri yenye mvuto wakati wa uimbaji wake. Baadaye muziki wa taarab ulisikika hadi Tanganyika (kwa sasa Tanzania) na kuanza kubuniwa na vikundi mbalimbali vya wanamuziki wa taarab. Khatib (1992) anaeleza kuwa, baadhi ya vikundi hivi ni pamoja na *Naad Ikhwan Swafaa* (1905), *Nadi Suub* (1908), *Michezani social club* (1954), *Culture Musical Club* miongoni mwa vingine. Muziki huu wa taarab vile vile ulisambaa kwa kasi ukaingia Dar es salaam, Tanga, Lamu hadi Mombasa.

Khatib (1992) anaeleza kuwa taarab asilia ilingia visiwani Zanzibar kwa madhumuni ya kumburudisha mfalme wa kipindi hicho Sayyid Said Bin Sultan pamoja na waandamizi wake. Anaeleza kwamba, Sayyid Said alikuwa mtu mpenda anasa na starehe na kamwe hangeishi bila kupata muziki wa taarab. Kila alipohitaji kupumzisha akili yake kipindi cha jioni na usiku, angechezewa muziki wa taarab.

Fair (2001) na Askew (2002) wanakubaliana kuwa kimsingi nyimbo za taarab zilitungwa kueleza masuala ya kijamii. Mikondo ya mijadala kuhusu ngazi za kijamii, masuala ya kijinsia na mahusiano ya kijamii vinajaribu kubadilishwa na watunzi wanapoviweka katika vifungu vya nyimbo za taarab. Wataalam hawa wanaeleza kuwa nyimbo hizi hutumia lugha ya kimafumbo kudhihaki hulka isiyokubalika na inayokiuka desturi za kijamii. Mbali na hayo nyimbo za taraab huwa na dhima ya kuonya, kusuta, kukashifu dhidi ya tabia hasi na kusifu zile chanya. Ujumbe unaoenezwa na nyimbo za taarab hutokana na uzoefu wa maisha, itikadi na mitagusano katika jamii na maisha kwa ujumla. Vilevile ujumbe katika nyimbo hizi huweka bayana uhusiano uliopo baina ya jamii na asasi mbalimbali za kijamii kama vile utamaduni (Yego, 2013).

Ni kutokana na uhusiano huo ndipo mtafiti amebaini kuwa zipo nyimbo za taarab ambazo maudhui yake yanadhihirisha uhusiano mkubwa baina ya nyimbo hizo na utamaduni wa Waswahili unaohusu mafunzo ya unyagoni ambayo hutekelezwa na makungwi. Kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa, dhima ya kungwi ni kuwafundisha wanawali masuala ya unyumba, basi uafiti huu umechunguza namna maudhui ya mafunzo ya makungwi yanajitokeza katika teule za taarab. Nyimbo zilizoteuliwa na mtafiti ni *Maji ya*

Uvuguvugu (Wachonga Vinyago), *Nenda salama* (Omar Kopa), *Ndoa* (Aslay na Khadija Kopa) na *Bi Harusi* (AT).

1.1 Suala la Utafiti

Nyimbo za taarab zimetafitiwa na wataalam mbalimbali kwa mitazamo tofautitofauti. Abdalla (2018) amechunguza dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Said Khamis naye Yego (2013) amechunguza nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taraab za Zanzibar. Makhulo (2015) ametafiti kuhusu mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taraab. Kutokana kwa kusoma kazi za awali, inabainika kuwa tafiti za awali kuhusu nyimbo za taarab, zimeegemezwa kwenye uchunguzi wa mafumbo katika taarab, masuala ya itikadi, nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taarab ni usimulizi wa pamoja na uchanganuzi wa taswira katika nyimbo za taarab. Suala la jumbe za nyimbo za taarab kufungamana na mambo ya kijamii yakiwemo utamaduni limetajwa tu kijuujuu katika tafiti zao. Kutokana na upekuzi wa kina wa mtafiti, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika baadhi ya nyimbo za taarab. Hili ni pengo ambalo utafiti huu ulizamia ili kuliziba.

1.2 Malengo ya Utafiti

Malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

- (i) Kubainisha dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili.
- (ii) Kuchunguza maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab.

(iii) Kutathmini mwingiliano kati ya dhima ya kungwi katika jamii na maudhui katika nyimbo teule za taarab.

1.3 Maswali ya Utafiti

- (i) Ni ipi dhima ya kungwi kwa katika jamii ya Waswahili?
- (ii) Ni maudhui yepi ya ukungwi yanayojitokeza katika nyimbo teule za taarab?
- (iii) Ni kwa jinsi gani dhima ya kungwi katika jamii inaingiliana na maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab?

1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuweka wazi dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili. Kwa kuenda nyanjani na kuwahoji baadhi ya makungwi katika jamii ya Waswahili ukanda wa Pwani ya Kenya, mtafiti aliweka bayana dhima yao ambayo huenda haijapata kuandikiwa kwa kina. Kando na hayo utafiti huu unatarajiwa kuonyesha kuwa wanawali wanaokosa fursa ya kufundishwa na kungwi kwa sababu moja au nyengine wanaweza kupata mafunzo hayo katika nyimbo teule za taarab. Aidha utafiti huu ni nyenzo bora ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Waswahili unaohusu masuala ya unyago.

Mbali na hayo, utafiti huu unakuza taaluma ya fasihi linganishi kwa kuwa unajaribu kulinganisha kipera cha mawaidha na kile cha nyimbo katika fasihi simulizi. Mawaidha yanayotolewa na kungwi kwa wanawali yanalinganishwa na kipera cha nyimbo (hususan za taarab). Utafiti huu vilevile umeweka msingi bora kwa watafiti wa baadaye kutanua

uwanda huu wa makungwi na nyimbo za taarab kwa kushughulikia vipengele vyake vingine.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kingei (1993) anasema kuwa kuna uhusiano baina ya nyimbo za taarab na utamaduni. Kama itakavyoelezwa mbeleni, nyimbo za taarab huhusishwa sana na jamii ya Waswahili nao utamaduni wa sherehe za unyago unahusishwa na Waswahili vilevile. Kwa kuwa taarab na utamaduni wa unyago vipo katika jamii ya Waswahili basi upo uwezekano mkubwa wa baadhi ya watunzi wa taarab kuimba mambo ya unyagoni. Kutokana na haya, mtafiti alipata msukumo wa kuchunguza namna mafunzo ya kungwi katika utamaduni wa unyago yanavyotekelezwa na baadhi ya nyimbo za taarab katika jamii ya Waswahili.

Pia, uhamiaji wa wanajamii kutoka mashambani kuenda mjini kutokana na sababu mbalimbali umechangia wao kukosa muda wa kutekeleza baadhi ya mila na desturi za kijamii kama kupata mafunzo ya unyagoni. Utafiti kuweka bayana mafunzo haya ya unyagoni yanavyotekelezwa na baadhi ya nyimbo za taarab, wanajamii wa Uswahilini watafaidika pakubwa. Hivyo basi, wanaokosa muda wa kupatana na kungwi kwa sababu moja au nyingine wanaweza kuyapata mafunzo ya kungwi katika nyimbo teule za taarab.

Aidha, kwa kuwa nyimbo teule za taarab zina mafunzo mengi kwa wanawali kuhusu ndoa, mtafiti alipata mshawasho wa kuteua mada hii ili kuwafaa wanawari kwa mafunzo anuwai kuhusu ndoa.

1.6 Upeo na Mipaka

Zipo tanzu nyingi za fasihi simulizi kama hadithi, semi, mazungumzo, ushairi na maigizo. Hata hivyo utafiti huu umejikita kwa tanzu mbili ambazo ni ushairi na mazungumzo. Hata hivyo, si vipera vyote vya tanzu hizi kwa ujumla bali utajikita tu kwa kipera cha mawaidha chini ya utanzu wa mazungumzo na kipera cha nyimbo chini ya utanzu wa ushairi simulizi.

Mbali na hayo, wapo watunzi (waimbaji) wengi wa nyimbo za taarab wakiwemo, Siti Binti Saad, Bi. Kidude, Juma Balo, Shakila Saidi Khamisi, Mwanaidi Shaaban na wengine wengi. Hata hivyo, utafiti huu utajikita tu kwa waimbaji wa taarab teule ambao ni Wachonga Vinyago, Omar Kopa, A.T, Khadija kopa na Aslay. Waimbaji hawa waliteuliwa na mtafiti kimaksudi kutokana na jumbe katika nyimbo zao teule zinazofungamana na utamaduni wa unyagoni wa Waswahili.

Aidha, utamaduni wa sherehe za unyagoni hutekelezwa katika jamii ya Waswahili wa Pwani ya Afrika Mashariki ambapo kungwi huwapa wanawali mafunzo ya unyumba. Si makungwi kutoka jamii yote ya Waswahili waliohojiwa bali makungwi kutoka eneo la Msambweni, kaunti ya Kwale kwa sababu makungwi wa eneo hilo la Msambweni hutumia kipindi kifupi kutoa mafunzo ya unyago ikilinganishwa na wa sehemu zingine. Pia, Msambweni ni eneo la mashambani ambalo halijaathiriwa sana na usasa wa mijini.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Tafiti mbalimbali zilifanywa kuhusu nyimbo za taarab huku kila moja wapo ikichukua mkabala tofauti. Ufuatao ni muktasari wa tafiti za awali ambazo zinatoa mchango kwa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Sauda (2022) alichunguza taswira katika nyimbo za taarab za kimahaba za Khadija Kopa. Kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki, alibaini kuwa nyimbo za kimahaba za Khadija Kopa zinatamia taswira mbalimbali kama vile za kiteolojia, kizuelojia kijiolojia na taswira za vitu vya kawaida. Kando na hayo, utafiti huu uliweza kuibua na kuweka dhahiri miktadha mbalimbali inayopelekea kuwepo kwa taswira hizi. Miktadha hii ni miktadha ya kiutamaduni, utandawazi, imani na ya kifasihi. Utafiti huu ulitufaa kinadharia kwa kuwa ulitumia nadharia ya Simiotiki kuchanganua nyimbo za taarab.

Abdallah (2018) alichunguza dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Said Khamisi. Katika utafiti wake alitumia nadharia ya mwikitiko wa msomaji na nadharia ya Simiotiki. Utafiti ulibainika kuwa kuna dhamira kadha wa kadha zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Said Khamis. Dhamira hizi ni pamoja na mapenzi, usaliti, utamaduni, elimu, dini, ukombozi na nyingine nyingi. Mtafiti amethibitisha kuwa dhamira ya utamaduni katika wimbo wa *Sasambu* wa Shakila Said imedhihirisha mambo ya mafunzo kwa Bi harusi. Mafunzo haya ni pamoja na namna ya kuishi maisha ya ndoa. Haya yaliwekea mtafiti msingi wa kuchunguza mafunzo ya utamaduni wa unyago kwa mwanamwali yanayotekelezwa na kungwi katika jamii ya Waswahili. Hata hivyo utafiti wa Abdalla unatofautiana na huu kwa kuwa wake unajikita kwa kipengele cha dhamira

na fani katika nyimbo za taarab ilihali utafiti huu ulijikita kwenye dhima ya kungwi katika nyimbo za taarab.

Misoi (2022) ametafiti kuhusu dhima ya usimulizi katika uwasilishaji wa nyimbo za taarab. Aliongozwa na nadharia ya Naratolojia. Kipengele cha wakati katika usimulizi ndicho kilichozingatiwa katika utafiti huo. Kupitia kwa kipengele hiki, maudhui ya mapenzi, utamaduni, ndoa, ukatili, usaliti na miongoni mwa mengine yalijadiliwa. Ufafanuzi wa maudhui ya utamaduni na ndoa katika utafiti huu ulitufaa katika kuweka msingi wa utafiti wetu. Utamaduni wa Waswahili unaohusisha masuala ya ndoa na unyago ndio uliozingatiwa katika utafiti wetu kwa kujikita kwenye mafunzo yake.

Kirimi (2015) naye amechunguza mabadiliko katika sherehe za unyago na ukeketaji za jamii za Waswahili wa Mumias. Katika utafiti wake alibaini kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa katika utamaduni wa unyago na ukeketaji wa Waswahili wa Mumias ambapo njia mbadala ya ukeketaji inatumika kwa mabinti. Waswahili wa Mumias wameishia kuasi ukeketaji wa wasichana katika sherehe za unyago na kuzamia kwa mafunzo ya unyumba pekee yake. Utafiti huu unabainisha wazi mambo yanayotekelezwa katika kuwapitisha wasichana katika kiwango hiki cha maisha. Mambo haya ni kucheza kwa ngoma za unyagoni na kuwapa wanawali mafunzo ya unyumba. Utafiti huu umetuwekea msingi kuhusu mafunzo ya unyumba wanyapokezwa wanawali.

Nyongesa (2022) ameshughulikia uchanganuzi wa mafumbo katika nyimbo teule za taarab za Siti Binti Saad. Katika utafiti wake, aligundua kuwa maana ya mafumbo katika nyimbo za mwanamuziki huyu yamefungamanishwa na utamaduni wa Waswahili wa

pwani ya Afrika Mashariki. Ili kuelewa mafumbo katika nyimbo hizi za taarab, ni bora mtafiti kuelewa utamaduni wa msanii vyema. Kwa kufanya hivi, mtafiti aliweza kufahamu na kuweka bayana maudhui yanayoelekezwa kimapumbo katika nyimbo hizi kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki. Kazi hii ilikuwa na manufaa kwetu kufahamu namna ya kuchanganua mafumbo katika nyimbo teule za taarab kwa kutumia nadharia ya Simiotiki ili kupata ujumbe unaobebwa na nyimbo hizo.

Ali (2018) ametafiti kuhusu matumizi ya ishara katika nyimbo teule za taarab za Mohammed Ahmed Mohammed. Ali (keshatajwa) ameweka bayana kuwa mtunzi wa nyimbo za taarab hutumia ubunifu wa hali ya juu kueleza mambo ya jamii yake katika tungo zake. Kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki mtafiti anaweka dhahiri namna Mohammed Ahmed amezungumza mambo ya jamii katika nyimbo zake kwa kutumia lugha ya ishara. Utafiti huu umekuwa na manufaa kwetu kinadharia na kwa kutufahamisha namna watunzi wanavyozungumzia masuala katika jamii na katika nyimbo zao.

Mbwana (2016) naye alitafiti kuhusu mabadiliko ya matumizi ya nyimbo za harusi za Kipemba kwenda katika kasida za harusi. Katika utafiti wake aligundua kuwa kuna mfanano mkumbwa wa kimuktadha na kidhima kati ya nyimbo za Kipemba na kasida za arusi. Kinacholeta mshahaba wa mfanano huu ni mazingira, shughuli za kawaida za Uswahilini na utamaduni. Uchunguzi wa dhima ya nyimbo hizi na kuiwekwa wazi na utafiti huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa kuchunguza dhima ya kungwi katika nyimbo teule za taarab.

Tafiti za awali zimeshughulikia vipengele mbalimbali katika nyimbo za taarab. Vipengele hivi ni pamoja na taswira, mafumbo, usimulizi, fani, dhamira, mabadiliko ya kihistoria katika uwasilishaji wa taarab, maudhui miongoni mwa vingine. Ni dhahiri kuwa suala la maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab halijashughulikiwa na watafiti wa awali. Hili linaibua pengo ambalo mtafiti alipania kuliziba.

1.8 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili, nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Uamilifu.

1.8.1 Nadharia ya Simiotiki

Nadharia hii iliasisiwa na Ferdinand Dassaussure (1913) na Charles Pierce (1977). Dassaussure alieleza kuwa katika matumizi ya lugha kuna kitaja na kitajwa ila hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kitajwa ila kuna ishara, picha, taswira au misimbo. Kuna aina tano za misimbo kwa mujibu wa Barthes (1994), msimbo wa kihemenetiki, kimatukio, kiseme, kiishara, na wa kirejelezi.

Msimbo wa kimatukio ni msimbo unaohusu utokeaji wa visa na matukio na kuwa wa kialama au kimsimbo. Kwa mfano, fisi ameingia sebuleni kauli hii haihusu fisi bali mtu aliye na sifa za fisi.

Msimbo wa kisemantiki unahusu taharuki ambapo humfikirisha msomaji juu ya kile anachodhamiria kukisoma au kukitafiti. Msimbo huu humjengea mtafiti taharuki ya kutaka kujua kwa nini msanii ametumia maneno hayo? Yanahusiana vipi na muktadha? Mhimili huu umetuongoza katika utafiti wetu kwa kumfanya mtafiti kujua maana ya

maneno yaliyotumika katika nyimbo teule za taarab na namna inayvohusiana na muktadha.

Msimbo wa kirejelezi nao hujengwa kutokana na viashiria vya utamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi ya kifasihi husika. Hujenga uhalisi maalum kutokana na matumizi ya vitu fulani ambavyo vinaeleweka na msomaji wa kazi ya kifasihi. Hii huipa kazi fulani za misingi ya utamaduni. Mhimili huu umetuongoza katika kuchunguza viashiria vya kitamaduni katika nyimbo teule za taarab na namna vinavyoibua dhima za kitamaduni za ukungwi.

Msimbo wa kiseme unatokana na neno sema. Neno sema linatumiwa kueleza elementi nasibishi ya kisemantiki ambazo hutuwezesha kupata picha fulani. Kutokana na viashiria fulani, kuelewa sifa kamili ya jambo hali au tukio fulani la kifasihi hutokea. Wamitila (2002) anatilia mkazo kuwa, semantiki hueleza kuwa vitu huwa na maana ya msingi na maana ya ziada.

Kifasihi msimbo wa kiseme hutumika kujenga lengo na maudhui kwa kutumia maneno ambayo yanatoa ukaribu wa maana ya kimsingi ya neno hilo na kile kinachorejelewa na neno hilo kifasihi. Wright (1975). Mhimili huu umetufaa katika kuchunguza namna maneno katika nyimbo teule za taarab yanajenga dhamira na maudhui ya mafunzo ya ukungwi.

1.8.2 Nadharia ya Uamilifu

Wallace na Wolf (1980) wanaeleza kuwa, nadharia hii, iliasisiwa na Emile Dukheim (1912). Wataalam hawa wanaeleza kuwa, nadharia hii iliendelezwa na waitifaki mbalimbali wakiwemo Radcliffe Brown (1952), Amitai (1993) na Alexander (2003).

Kwa mujibu wa Bascom (1954) vipengele vya fani katika utanzu wowote wa fasihi hutumiwa katika mazingira mbalimbali kwa madhumuni ya kutekeleza dhima mbalimbali.

Nadharia ya uamilifu unasisitiza kuwa uchambuzi wa dhima zinazojitokeza katika kazi ya fasihi. Fasihi ina tanzu na vitanzu vyake ambapo kila kitanzu kina dhima yake katika jamii. Hii ndiyo nguzo kuu ya nadharia hii. Hivyo basi, mawaidha ya kungwi ni kitanzu cha mazungumzo katika fasihi simulizi na kina dhima yake katika jamii. Nadharia hii imetuongoza katika utekelezaji wa lengo la kwanza kubainisha dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili.

1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inahusu eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli ukusanyaji na uchambuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

1.9.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika maktabani na nyanjani. Maktabani mtafiti amesoma tasnifu, makala na kupekua mtandaoni ili kujifahamisha masuala ya kinadharia, mbinu za utafiti na hata kuisoma na kuelewa data yake ya nyimbo teule za taarabu. Nyanjani mtafiti alitembelea eneo la pwani ya Kenya ambako kuna makungwi ambao wanaendeleza utamaduni wa mafunzo ya unyagoni kwa wanawali. Mtafiti aliwasaka makungwi hawa katika eneo la Msambweni Kaunti ya Kwale na kuwahoji ili kupata dhima yao.

1.9.2 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ulifanyika kwa njia ya usampulishaji wa kimaksudi. Eneo la Msambweni lilitolewa kimaksudi na mtafiti ili kuwahoji makungwi wa eneo hilo. Hii ni kwa sababu eneo hilo ni la mashambani wala halijaathirika sana na usasa wa maisha ya mijini hivyo utamaduni wa unyago bado umeshikiliwa kwa sana. Makungwi waliohojiwa na mtafiti waliteuliwa kwa njia ya usampulishaji wa kimaksudi ambapo wale wanaofahamika kijijini ndio waliohojiwa. Kungwi wanne waliteuliwa kimaksudi na mtafiti kisha kuhojiwa.

Aidha wapo waimbaji wengi wa nyimbo za taarab kama vile; Siti Binti Saad, Bi Kidude, Juma Balo, Mwanahawa Binti Ali na wengine wengi. Hata hivyo waimbaji wanne pekee ndio walioteuliwa na nyimbo zao teule kutengwa kutumiwa katika utafiti. Waimbaji hawa walioteuliwa ni Wachonga Vinyago, Omari Kopa, AT, Khadija Kopa na Aslay.

Nyimbo zao teule zilizotumika katika utafiti huo ni; *Maji ya Uvuguvugu* (Wachonga Vinyago), *Nenda salama* (Omar Kopa), *Ndoa* (Aslay na Khadija Kopa), *Bi Harusi* (AT). Nyimbo hizi ziliteuliwa kimaksudi na mtafiti kutokana na jumbe zake ambazo zimefungamana na utamaduni wa mafunzo ya unyagoni ya Waswahili.

1.9.3 Ukusanyaji wa Data

Data ya maktabani ni nyimbo teule za taarab. Data hiyo iliyokusanywa na mtafiti kwa kupakua nyimbo hizo kutoka mtandao wa kijamii wa *youtube* kwa ajili ya uchanganuzi.

Data ya nyanjani ni maelezo ya makungwi kuhusu dhima yao katika mahojiano ya moja kwa moja na mtafiti. Data hii ilikusanywa na mtafiti kwa kurekodi mahojiano yake na makungwi kwa kutumia vifaa vya tepurekoda na simu. Mtafiti alinasa mahojiano hayo katika vifaa hivi kwa ajili ya kuichanganua.

1.9.4 Uchanganuzi wa Data

Data zilizokusanywa kutoka maktabani na nyanjani zitapangwa, kuelezwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti ili kuipa kazi ya utafiti mpangilio faafu. Haya yalifanyika kwa njia ya utaratibu kwa kuzingatia hatua mbalimbali;

Kwanza, mtafiti aliipanga data ya nyajani ambayo ni maelezo ya makungwi katika mahojiano kuhusu dhima yao. Mtafiti alisikiliza rekodi za mahojiano zilizonaswa huku akidondoa hoja muhimu na kupuuza maelezo ya ziada yasiyofaa kwenye mada. Maelezo ya makungwi wote waliohojiwa yalidondolewa huku hoja za dhima zao zenye usawa zikinakiliwa kwa kuambatanisha na dondoo za usemi wa moja kwa moja wa makungwi.

Pili, data ya maktabani ambayo ni nyimbo teule za taarab ilichanganuliwa kwa kuchambua jumbe katika nyimbo hizo zinazohusu maudhui ya ukungwi. Kisha, mtafiti alilingalisha jumbe hizo na dhima ya kungwi iliyoelezwa na makungwi katika mahojiano.

1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa matumizi ya maandishi ya matini yatakayopangwa katika aya. Dondoo za maelezo ya makungwi ziliambatanishwa na maelezo haya husika. Vilevile unakuzi wa baadhi ya mistari na vifungu vya nyimbo teule za taarab zilizotumika katika utafiti ulifanyika. Hayo yote yalifanyika kwa njia iliyo wazi inayodhihirisha utekelezaji wa malengo ya utafiti kwa kuongozwa na nadharia ya Simiotiki na ya Uamilifu.

1.10 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alipata vibali hitajika kabla ya kuingia nyanjani na kuzama katika utafiti. Atatafuta vibali kutoka kwa shule husika, kitengo cha *Center for Research Ethics and Safety (CRES)* pamoja na *National Council for Science and Technology and Innovation (NACOSTI)*. Mbali ya hayo mtafiti alihifadhi siri ya watafitiwa na kuwahakikishia uaminifu kwao. Aidha mtafiti amewatambua wataalam na watafiti wote ambao anaewanukuu na kushirikisha mawazo yao katika utafiti wake kwa kuwaorodhesha mwishoni mwa tasnifu.

SURA YA PILI

DHIMA YA KUNGWI KATIKA JAMII YA WASWAHILI

2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza imejikita kwenye vipengele muhimu ambavyo vimeuwekea msingi utafiti huu. Vipengele hivi ni pamoja na usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka. Aidha, tahakiki ya yaliyoandikwa kuhusu mada imefanywa ili kuchangia na kujenga utafiti huu. Vilevile, msingi wa nadharia umeshughulikiwa ili kuongoza utekelezaji wa malengo ya utafiti, mbinu ya utafiti pamoja na maadili ya utafiti vimeshughulikiwa.

Sura hii imeshughulikia dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili kwa kujikita kwenye mafunzo wanayotoa makungwi. Mijadala katika sura hii inahusisha data iliyokusanywa nyanjani; eneo la Msambweni katika kaunti ya Kwale nchini Kenya. Data hii ilikusanywa kwa njia ya mahojiano na uchunzaji ambapo mtafiti aliwahoji makungwi wa eneo hili kupata kwa kina mafunzo wanayotoa kwa wanawali kama dhima yao kuu. Kwa njia ya uchunzaji, mtafiti aliweza patana na kungwi katika mazingira halisi ya kutolea mafunzo kwa wanawali na kushiriki zoezi hilo. Kwa kuwa suala kuu linalojadiliwa katika sura hii limejikita katika utamaduni wa Waswahili, historia fupi ya utamaduni wa Waswahili imetolewa ili kufafanua kiini cha mafunzo ya kungwi unyagoni katika jamii ya Waswahili. Sehemu ya mwisho katika sura hii ni mijadala inayohusu data iliyokusanywa nyanjani kuhusiana na dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili.

2.1 Historia Fupi ya Utamaduni wa Waswahili

Waswahili ni jamii ya watu wanaoishi kwenye Pwani ya Afrika Mashariki hususan katika maeneo ya Kenya na Tanzania. Historia ya utamaduni wao imejengeka katika mwingiliano wa tamaduni za Kiafrika, Kiarabu, Kihindi na Ulaya hasa kutokana na mabadiliko yaliyoletwa na biashara za utumwa, biashara ya hariri na athari za ukoloni (Wamitila, 2006). Msingi wa utamaduni wa Waswahili umejengwa juu ya mchanganyiko wa tamaduni za kiasili za Wabantu wa Pwani, Wahindi, Waarabu na baadaye Wazungu. Mazrui (1995) anasema kuwa uhusiano wa kihistoria wa Waswahili na Waarabu wa Uajemi umeathiri sana lugha, dini na sanaa zao.

Wamitila (2006) amejadili utamaduni wa Waswahili katika vitengo mbalimbali ambavyo ni lugha, dini, sanaa na fasihi, pamoja na mila na desturi. Mbaabu (1990) kwa upande wake anasema kuwa lugha ya Kiswahili ni kipengele muhimu cha utamaduni wa Waswahili, kwani inaunda msingi wa mawasiliano na ushirikiano kati ya watu wa jamii hii. Anasisitiza kuwa lugha hii ni zaidi ya chombo cha mawasiliano; ni alama ya utambulisho wa Waswahili na ni kipengele cha kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wao.

Mbali na lugha ya Kiswahili, dini ni mojawapo ya nguzo za utamaduni wa Waswahili. Hussein (2003) anasema kuwa utamaduni wa Waswahili umeathiriwa sana na dini ya za Kiislamu kutokana na mwingiliano wa kihistoria na Waislamu, Waarabu na Wahindi. Dini ya Kiislamu ilifika Pwani ya Afrika Mashariki kuanzia karne ya saba na ikawa na nafasi kubwa kijamii na kiasia. Tangu wakati huo Waswahili wengi walikubali dini hii na ikakuwa sehemu kubwa ya utamaduni wao.

Aidha, sanaa na fasihi vimejadiliwa na wataalam mbalimbali kama sehemu ya utajiri wa utamaduni wa Waswahili. Kulingana na wataalamu kama Mbaabu (1990), sanaa ya Waswahili inaonyesha uhusiano wa karibu kati ya tamaduni za Afrika Mashariki na za kigeni, hasa tamaduni za Waarabu na Wahindi. Sanaa ya Waswahili inaambatana na mila na desturi za jamii na inajumuisha sanaa za maandishi kama vile mashairi ya Kiswahili (mashairi ya kisanaa), uimbaji wa jadi, ngoma, na pia sanaa ya uchoraji inayohusiana na mapambo ya majengo, meli, na vifaa vya kijamii. Kwa mfano, utamaduni wa Waswahili unajivunia sanaa ya uchoraji na mapambo ya majengo, hasa katika maeneo ya pwani kama Zanzibar na Mombasa, ambapo sanaa ya kupamba majengo na madirisha ina alama za kipekee. Sanaa hii inahusisha maumbo ya kigeni na ya asili, na inatoa uhusiano kati ya historia ya Waswahili na utamaduni wa kijamii. Hali kadhalika, ngoma na uimbaji wa Waswahili, kama vile "ngoma za pwani" na "taarab," ni sehemu muhimu ya utamaduni huu, ikionyesha hisia na mitindo ya kijamii ya Waswahili.

Kwa upande mwingine, fasihi ya Kiswahili inahusisha mashairi na riwaya ambayo imetumika katika kueneza na kuenzi utamaduni wa Waswahili. Uandishi wa vitabu, hadithi za muktadha wa Waswahili, na mashairi ya Kiswahili ni sehemu muhimu ya utamaduni wa kijamii na kifasihi. Mbaabu anasema kuwa, mashairi ya kijadi ya Waswahili yalisimuliwa kama tenzi. Mifano ya tenzi hizi ni pamoja na *Utenzi wa Hamziya*, *Utenzi wa Mwana Kupona*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Al- Inkishafi* miongoni mwa zingine.

Kitengo kingine cha utamaduni wa Waswahili ni mila na desturi ambayo ina upekee wake ikilinganishwa na za jamii zingine. Mila na desturi za Waswahili zinajumuisha michezo ya jadi kama vile bao, ngoma za jadi na michezo ya maji. Pia Waswahili wana mila na desturi zao zinazohusu namna wanavyoendesha sherehe zao za harusi, unyago na jando. Kama anavyoeleza King'ei (2010), utamaduni ni tajiriba, maarifa, ujuzi, hekima ama busara ambayo mtu hujifunza katika jamii anamoishi. Ameuleza utamaduni katika viwango mbalimbali ambavyo ni mila na desturi, njia za kujielezea, njia za kuelimisha pamoja na malighafi. Mila na desturi ni imani, kaida na namna jamii huendesha shughuli zao za kawaida zikiwemo kuwapa watoto majina, ndoa, mazishi, matambiko, sherehe za jando na za unyago.

Mila na desturi ya unyago wa Waswahili ndicho kiini cha mijadala ya sura hii. Utamaduni wa unyago una historia ndefu ila ulipata kuenea zaidi tangu kuanzishwa kwa dini ya Uislamu katika maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki katika karne ya 9 na 10 (Hussein, 2003). Msomi huyu anazidi kueleza kuwa, dini ya Kiislamu ilileta mabadiliko katika desturi za kijinsia na kijamii hivyo unyago ukawa na uhusiano wa karibu na maadili ya dini hii. Unyago ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Waswahili ambapo unahusisha mabadiliko ya kijinsia, kujiandaa kwa maisha ya ndoa na uhamasishaji wa staha za kijamii (Juma, 2020). Unyago ni mchakato ambao umekuwa ukifanyika ndani ya vizazi vingi katika jamii ya Waswahili kwa madhumuni mapana ya kuandaa vijana kwa ndoa. Juma (keshatajwa) anazidi kueleza kuwa unyago unanua kumfundisha mvulana na msichana stadi za kijamii na za familia ambapo msichana hufundishwa

mapishi, usafi pamoja na malezi ya familia naye mvulana kufundishwa majukumu ya uongozi, kazi za kiume na mbinu anuwai za kuishi na familia kwa ufanisi.

Waswahili wanatambulika kwa sherehe za unyago ambapo wanawafunza wanawali kuhusu masuala ya ndoa, mafunzo ambayo hutekelezwa na kungwi au somo (Kirimi, 2014). Kutokana na haya, mafunzo ya kungwi kwa wanawali ambayo hutekelezwa katika sherehe za unyago yamejadiliwa kwa kina katika sura hii kama mila na desturi za jamii ya Waswahili. Mafunzo ya kungwi kwa wanawali ambayo ndiyo dhima yao katika jamii, ndilo suala kuu ambalo limeshughulikiwa kwa kina katika sura hii kwa kuongozwa na data maalum iliyokusanywa nyanjani.

2.2 Dhima ya Kungwi katika Jamii ya Waswahili

Dhima kuu ya kungwi katika jamii ya Waswahili ni kuwapa wanawali mafunzo kuhusu ndoa. Mafunzo haya wanaanza kuyatoa pindi tu mwanamwali amebalehe. Ijapokuwa wanawali wa kiume hupewa mafunzo haya, uzingativu mwingi upo kwa wari wa kike na kwa kigezo hiki ndipo tulijikita kwa mafunzo ya kungwi kwa wanawali katika jamii ya Waswahili. Nadharia ya Uamilifu ndiyo iliyotuongoza katika kukuza mijadala kuhusu haya. Mwanauamilifu Bascom (1954) anasema kuwa, vipengele vya fani katika utanzu wowote wa fasihi hutumiwa katika mazingira anuwai kwa madhumuni ya kutekeleza dhima mbalimbali. Aidha, fasihi ina tanzu na vitanzu vyake ambapo kila kitanzu kina dhima yake katika jamii. Mafunzo ya kungwi, ambayo ni mawaidha, ni kitanzu cha mazungumzo katika fasihi simulizi. Hivyo basi, kungwi na mafunzo yake ana dhima ya kuwashirikisha wanawali katika elimu ya vitengo vyote vya masuala ya ndoa au unyumba. Kutokana na mahojiano na makungwi wa eneo la Msambweni kaunti ya

Kwale, pamoja na uchunzaji, tumeweza kuyapata mafunzo haya na kuyajadili katika vitengo mbalimbali kwa kina. Vitendo hivi ni pamoja na namna ya kuhudumia mume, vitu vya kiasili na matumizi yake, namna ya kuzungumza na mume, mapishi, usafi, mapambo na namna ya kuzungumza na watu kwa ujumla.

2.2.1 Namna ya Kumhudumia Mume

Kumfundisha mwanamwali namna ya kumhudumia mume ndiyo dhima kuu ya kungwi katika jamii ya Waswahili. Lengo kuu la kungwi kumpokeza mwanamwali mafunzo haya ni kumsaidia kuidumisha ndoa yake ili asije kupata talaka. Anamkumbusha mwanamwali wajibu alionao kwa mumewe. Ili kupata undani wa jukumu hili, mtafiti aliwahoji makungwi lengwa na wakawa na haya ya kusema;

Mume anaporejea kutoka kazini, mke anapaswa kumkaribisha nyumbani kwa mahaba kwani atakuwa amechoka na huenda kukereka kazini. Anapoingia kwa nyumba, amlaki kwa kumkumbatia na kumwambia maneno matamu ya kimahaba kama vile, “Karibu ndani mume wangu, mimi hapa mkeo wa ndoa, ua lako na pambo lako la kuyafurahisha macho yako. Nikuhudumie vipi? Sijui utakula kwanza ama utakoga kwanza maana chakula ki tayari na maji ya kukoga ya vuguvugu nimeshayapeleka bafuni.” Maneno haya matamu yatamfanya mume kusahau kero zote za kazini na uchovu wa siku na kujihisi kuthaminiwa hivyo kulifufua penzi lake kwa mkewe tena.

Kauli hizi za kungwi katika dondoo hili sio tu nadharia kukosa kutumiwa bali pia zinaenda sambamba na mtazamo wa Rosenblatt (2018) anayedai kuwa, kulingana na muktadha na desturi za jamii, mke anastahili kumjengea mume hisia kila zinapovurugika kutokana na pandashuka za maisha. Haya yanachangia pakubwa katika ustawishaji wa uhusiano wa wote wawili. Mawaidha ya kungwi katika dondoo hili ya mke kumlaki mume, kumwambia maneno matamu ya kimahaba, kumletea chochote anachohitaji

miongoni mwa mengine yanalenga kuzindua hisia za kimahaba na kuondoa zile hasi zinazotokana na changamoto za maisha. Kwa kuwa jukumu kuu la mume katika ndoa ni kusaka tonge la familia basi ni dhahiri kuwa katika kuhangaikia hili anakumbana na changamoto nyingi ambazo zingine ni za kukatisha tamaa na zingine za kuvuruga hisia. Hii ndio sababu ya kungwi kumuelimisha mke kuhusu mbinu mbalimbali za kuzindua hisia hizi za kimahaba.

Kando na huduma kwa mume anaporejea nyumbani, kungwi aliweza kufafanua jukumu lake la kumfundisha mwanamwali wa kike kuhusu anachostahili kumfanyia mumewe anapojiandaa kuondoka asubuhi kutafuta riziki. Kuhusiana na undani wa suala hili, mmoja wa makungwi lengwa aliyehojiwa alitoa maelezo yafuatayo;

Mume anaporauka kujiandaa kuenda kazini, ni jukumu la mke kuhakikisha kuwa amempelekea maji bafuni ambayo ni ya vuguvugu iwapo kuna baridi kisha kumpa kitambaa cha kufuta maji mwilini baada ya kuoga. Wakati anapooga amchagulie vazi la kuvaa na kulipiga pasi wala sio kumruhusu avae vazi lililojikunja kama lililotolewa mdomoni mwa ng'ombe akilitafuna. Pia avifute viatu vyake vumbi na kumwandalia kiamsha kinywa.

Maelezo haya ya kungwi yanamsawiri mke bora kama mwajibikaji na mwenye bidii ili aweze kutekeleza haya yote kwa wakati hasa kama yeye pia anatoka kusaka riziki. Ingawa wafeministi kama vile Beauvoir (1994) huushambulia utamaduni huu kwa kusema kuwa ndoa humdunisha mwanamke, kungwi anamkumbusha mwanamke wa Uswahilini majukumu yake katika ndoa si utumwa bali ni wajibu. Anaonyesha kuwa katika karne ya sasa mwanamke ana uhuru wa kufanya kazi na kushirikiana na mume katika kusaka riziki ila hapaswi kuusahau wajibu wake kwa mumewe. Mtafiti aliweza kuwahoji makungwi

wa eneo la Msambweni kuhusu msingi wa mafunzo haya na kubaini kuwa wanajamii wanaongozwa sana na amali za jamii ya Waswahili pamoja na mafunzo ya *Utenzi wa Mwanakupona* ulio na mafunzo mengi kuhusu majukumu ya mke katika ndoa.

Njia nyingine ya kumhudumia mume ni kumwandalia chakula. Kama ulivyo msemu kuwa mtoto hutazama kisogo cha ninake, ni wazi kuwa msichana anapokuwa hujifunza kazi nyingi za nyumbani kama vile kupika kwa kumtazama mamake anavyopika. Mapishi mazuri ndiyo anayosisitiza kungwi katika mafunzo yake kwa mwanmwali. Katika mahojiano na kungwi, alisema haya kuhusu mapishi.

Mke ana jukumu muhimu sana la kumwandalia mumewe chakula kitamu na kwa wakati sahihi. Iwapo ana kijakazi nyumbani kwake, basi ajitahidi sana chakula cha mumewe akiandae na kumpakulia mwenyewe. Chakula chenyewe kiwe kitamu na kilichotiwa viungo vya kiasili kama vile nazi au iwapo ni chai, ikolezwe viungo kama mdalasini, iliki, tangawizi, karafuu na vinginevyo. Chakula kitamu humnata mume asitamani kula kwingine bali kile kile cha mkewe.

Katika dondoo hili, mambo kadha wa kadha yanajitokeza la msingi likiwa mwanamke kujua namna ya kupika vyakula vya aina mbalimbali. Jambo jingine ni kumuandalia mume chakula ni ishara ya mapenzi kwake kwani mume atakuwa akitazamia kurejea nyumbani ili akile chakula cha mkewe. Hili linawangandisha wanandoa pamoja iwapo mke atamwachia kijakazi jukumu hili la kumwandalia mumewe chakula basi huenda mapenzi yakahamishwa kwake.

Mbali na hayo, mke anatarajiwa kumtengea mumewe muda ili kustawisha ndoa. Wakati mume anaporejea nyumbani baada ya shughuli za siku, anatarajia kutumia muda huo na mkewe ili kuyahuisha mahusiano yao. Kungwi alipoulizwa kuhusu dhima yake

nyingine, alieleza kuwa, humfundisha mwanamwali wa kike kuhusu namna ya kutumia muda wake vizuri na mumewe katika ndoa. Alisema kuwa;

Wanawake wengi wanapopata watoto katika ndoa huwasahau waume zao kabisa na kujishughulisha tu na watoto wao. Wakumbuke pia mume ni kama mtoto na anastahili kuangaliwa au kuhudumiwa pia. Zaidi ya kumshughulikia mtoto au watoto, mke anapaswa kutenga muda wake na mumewe. Kwa mfano, watoto wanapokula na kuenda kulala, huu ndio muda anapaswa kumburudisha mumewe kwa kucheza naye, kukimbizana chumbani, kumkanda na hata kutaniana naye. Pia afahamu kuwa simu ndio sumu kubwa katika ndoa. Wanapoingia chumba cha kulala, asishinde muda wote katika mitandao ya kijamii hadi usiku wa manane.

Kauli hii ya kungwi inamulika sana jamii ya kisasa ambapo kuna wimbi kubwa la matumzi ya mitandao ya kijamii ambayo inajenga uraibu. Kirkpatrick (2021) analizungumzia kwa kina swala hili la muda wa matumizi ya mitandao ya kijamii katika ndoa. Anasema kwa wanandoa wanapokuwa na wakati mwingi sana kwenye mitandao ya kijamii, hupunguza sana muda wa mawasiliano ya ana kwa ana baina yao. Kushinda sana kwenye mitandao ya kijamii humfanya mmoja wa wapenzi kuanza kuhisi kutengwa. Hili huathiri ndoa kwa njia hasi mno na huweza hata kuchangia kusambaratika kwake. Hivyo, kungwi humuonya mwanamwali wake kuhusu kukubali kutekwa na mitandao ya kijamii na kumpuuza mumewe asije akachangia kuvunjika kwa ndoa yake.

2.2.2 Mafunzo ya Vifaa na Maana yake

King'ei (2010) katika ufafanuzi wake wa asasi ya utamaduni, anataja malighafi kama mojawapo ya mawanda ya utamaduni. Ameeleza malighafi kama kazi ya kiufundi ambazo ni za kutengeneza vifaa mbalimbali vya kiasili kama vile vinyago, kinu, mchi, mbuzi, shanga, kanga, vikuku, ufagio, zana za vita kama uta na vinginevyo. Uchongaji au utengenezaji wa vifaa hivi ni maarifa ambayo mtu hujifunza kutoka jamii yake. Vifaa hivi ni kitambulisho cha jamii mahususi hivi kwamba, zipo jamii zinazotambulika kwa uchongaji, uchoraji, ufinyanzi, ususi miongoni mwa ufundi mwingine Kupitia mahojiano ya mtafiti na makungwi lengwa, waliweza kuweka bayana kuwa vifaa hivi vina majukumu maalumu katika ndoa. Hivyo basi, jukumu lao ni kuwafundisha wanawali kuhusu majukumu fiche ya kila kifaa katika ndoa na namna ya kukitumia. Sehemu inayofuata ni mijadala kuhusu maelezo ya makungwi kuhusiana na vifaa maalum na maana yake.

2.2.2.1 Matumizi ya Mbuzi

Kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2013), mbuzi ni kifaa cha kukunia nazi. Kifaa hiki kina sehemu ya mbao upande wa nyuma na sehemu ya msumeno upande wa mbele ambayo ndiyo hukuna nazi. Mbuzi hutumiwa sana na Waswahili wa Pwani ya Afrika Mashariki kwa sababu ya kuwepo kwa minazi kwa wingi katika eneo hilo. Asilimia kubwa yao hutumia nazi kama kiungo cha kutia ladha na harufu tamu katika vyakula mbalimbali kama vile maharage, wali, mboga miongoni mwa vingine. Mmoja wa makungwi lengwa alipohojiwa kuhusu namna wanavyowafunza wari kuhusu njia mwafaka ya kukuna nazi, alieleza ifuatavyo;

Nazi huvunjwa kisha kukunwa kwa utaratibu na ustaarabu wala sio kwa fujo kama mgurumo wa trekta. Unapokuna kwa ustaarabu, hutawakera majirani na kelele hasa ukiwa unaishi kwa vyumba vya kupanga. Unapomaliza kukuna unaweka katika kufumbu na kisha uongeze maji kidogo na kuisukasuka ili kupata tui. Tui ya kwanza huitwa tui bubu na ina mahali pake maalum inapowekwa tofauti na tui ya pili. Baada ya kukamilisha shughuli nzima ya ukunaji nazi, sehemu ya mbuzi ya msumeno inapaswa kusafishwa kuondoa machicha ya nazi.

Maelezo haya ya kungwi yanamlenga sana mwanamke wa Uswahilini ambaye anapaswa kufahamu namna ya kutekeleza zoezi hili kwani chakula kingi anachotarajia kumwandalia mumewe kinapaswa kutiwa nazi. Hata hivyo, zoezi hili la ukunaji nazi kwa kutumia mbuzi halihusishi tu maana haya ya kimsingi pekee bali kuna maana fiche. Kulingana na kungwi huyo, kukuna nazi ni jazanda. Wanawafunza wanawali kuwa kukuna nazi kijazanda ni tendo la ndoa ambalo halihitaji kuparamiwa kwa fujo na kelele nyingi ili kuepuka kuwakera majirani. Aidha, walieleza kuwa kusafisha machicha kwenye mbuzi baada ya zoezi la ukunaji nazi kunarejelea usafi unaopaswa kuzingatiwa baada ya tendo la ndoa. Njia hii wanayotumia makungwi kuwafundisha wanawali wa kike inathibitisha maoni ya Gentner na Forbus (2011) wanaodai kuwa ufunzaji mzuri ni wa kutumia analogia ya vitu faafu vilivyo halisi kurejelea vilivyo dhahania. Wataalam hawa wanaeleza kuwa, unapotumia vitu vinavyofahamika katika mazingira ya mwanafunzi kama analogia ya vitu vya kidhahania (asivyovifahamu), humfanya mwanafunzi kuelewa zaidi. Uelewaji huu unatokana na mwanafunzi kujenga taswira ya kitu dhahania kwa kuhamisha maelezo ya kitu halisi kwacho. Hivyo basi, makungwi hawa wanapotumia analogia ya mbuzi na ukunaji nazi humwezesha mwanamwali kuelewa maana dhanishi (ya kimsingi) na maana kimatilaba (ya ziada) ambayo kwao ni dhahania kwa kuwa hawajashiriki kitendo hicho kabla ya kuingia ndoani.

2.2.2.2 Matumizi ya Ufagio

Hiki ni kifaa kinachotengenezwa kwa vitu kama vile nyasi au makuti kwa ajili ya kuondolea taka sakafuni. Kwa kuwauliza makungwi lengwa kuhusu mafunzo wanayowapa wanawari kuhusu ufagio, walisisitiza kuhusu ufagio wa kiasili (kijadi) unaotengenezwa kwa nyasi au makuti wala sio ufagio wa kisasa wenye kijiti kirefu ambapo mtu hufagia akiwa wima. Walisema kuwa ufagio wa kiasili ulio mfupi ndio unaopaswa kutumiwa na mwanamke aliye katika ndoa wakati wa shughuli ya kufagia.

Kwa udadisi wa kutaka maelezo ya kina kuhusu haya kungwi alieleza yafuatayo;

Tunapomfundisha mwanamwali wa kike kuhusu matumizi ya ufagio, tunamwambia moja kwa moja kuwa, si lazima sebule au chumba chochote kiwe kichafu ndipo uchukue ufagio kuanza kufagia. Mume anaporejea nyumbani machweo, baada ya maakuli anaweza akawa anatazama televisheni au yuasoma gazeti basi mke nawe unapaswa kuwa mbunifu kulizindua penzi ndani yake. Utachukua ufagio mfupi na kuanza kufagia huku ukiwa umeinama mbele yake na kuchezechesheshesha mwili kusudi likiwa “kumchokozachokoza” tu. Ishara na miondoko hizi za mwili ziambatane na kumtupia jicho la pembeni mara kwa mara na ndipo hapo utasikia akitoa kikohozi hafifu cha kulazimisha na kukuomba umletee kitu chochote kama vile wembe chumbani. Pindi tu unapoingia chumbani, atakufuata humo.

Kuwasiliana kupitia ishara na miondoko ya mwili ni njia inayojumuisha matumizi ya alama, ishara na mienendo ya mwili kuwasilisha ujumbe. McNeill (2005) anasema kuwa, miondoko ya mwili na matumizi ya ishara kama kukonyeza jicho, tabasamu na zingine, hutumika kuwasilisha mawazo na hisia mbalimbali na hili humfanya mpokezi kuelewa ujumbe fiche unaokusudiwa. Haya yanajenga maelezo ya kungwi katika dondoo kuwa, kufagia kwa miondoko mbalimbali na ishara kuna dhima ya kuwasilisha mawazo na hisia za mke kwa mumewe. Kufagiafagia na kumfanyia mume vitendo vya ‘uchokozi’ ndio

ubunifu ambao kungwi wanawafundisha wanawari wa kike kuutumia katika ndoa ili kuyahuisha mapenzi kati ya mume na mke.

2.2.2.3 Matumizi ya Kanga

Kulingana na Mchomeki (2023) kanga ni nguo ya kitamaduni yenye rangi angavu na ujumbe wa maandishi yaliyoshonwa inayotumiwa kwa sana nchini Tanzania na maeneo mengine ya Afrika Mashariki. Aghalabu kanga huvaliwa na wanawake lakini pia wanaume wanaweza kuvaa. Mchomeki analeza kuwa kanga inawakilisha urithi wa utamaduni wa jamii na ina majukumu makubwa ikiwa ni pamoja na kuwa ishara ya kitambulisho cha jamii na mawasiliano ya kijamii. Katika mahojiano ya mtafiti, makungwi lengwa walisema kuwa kanga ni mojawapo wa vifaa wanavyojihami navyo wakati wa kumfundisha mwanmwali. Waliyafafanua matumizi ya kanga kama ifuatavyo;

Mke na mume wanafaa kuwa na doti kadhaa za kanga chumbani mwao. Wanapoingia chumbani, wanapaswa kuvaa kanga wala sio vazi lingine. Ni jukumu la mwanamke kuchagua aina na rangi ya kanga kulingana na maudhui ya usiku huo. Kanga itakayochaguliwa iwe na maadishi yanayoendana na maudhui ya usiku huo, kama vile, ‘hizi zako zabibu, kula taratibu,’ au ‘nakupenda mume wangu.’ Kwa upande mwingine iwapo mume alimkosea mke wake kwa njia yoyote ile mbeleni basi anapoingia chumbani atachagua kanga yenye ujumbe mzito kama vile; ‘nisamehe mke wangu, nakupenda si utani.’ Kuomba msamaha kunaruhusiwa tu katika chumba cha kulala kupitia maneno pekee wala sio kuzungumza kwani ni marufuku kusuluhishia migogoro ya ndoa kitandani.

Mchomeki (2023) alifanya utafiti kuhusu kanga kama ishara ya utamaduni kama vazi linalotumika kama chombo cha mawasiliano. Katika utafiti wake, alisema kuwa kanga inatoa nafasi kubwa ya kueleza mawazo, maoni, hisia na ujumbe kwa ujumla bila mtu kutamka neno lolote. Ujumbe huu unaweza kuwa wa kimapenzi, kidini, kifalsafa ama wa

kijamii. Maelezo haya ya Mchomeki yanaendana na yale ya makungwi lengwa katika dondoo hili ambao wanasisitiza kuhusu ujumbe wa kuibua hisia za mapenzi unaowasilishwa na kanga. Mume anaposoma ujumbe ulio kwenye kanga ambalo mkewe amevalia kama, ‘hizi zako zabibu kula taratibu’ ataweza kufasiri na kuelewa ujumbe huo bila hata kuambiwa chochote na mkewe. Bila shaka atajua anacholenga mkewe naye hatajukumika kumfariji mumewe kwa mahaba. Kwa upande mwingine, naye mume anapokuwa amekosea mkewe mbeleni hatatakiwa kuzungumza wanapokuwa na mkewe chumbani bali atavaa kanga enye maandishi ya *nisamehe mke wangu, nakupenda si utani*. Ujumbe huu ni wenye hisia nzito kwa moyo na taratibu utaibusha hisia za msamaha kwa mke hali kadhalika za mapenzi.

2.2.2.4 Matumizi ya Shanga

Shanga ni vitu vya mapambo vyenye umbo la duara vinavyotengenezwa kwa kutumia vifaa mbalimbali kama vile plastiki, mbao, vioo au vyuma (Harris, 2017). Shanga zinatumika kama nyenzo za mawasiliano, kama kazi za sanaa, ishara ya utambulisho wa kitamaduni na mapambo kwa ujumla. Harris anaeleza kuwa, shanga hutumiwa katika sherehe na mafunzo ya ndoa yanayofanywa na masomo au makungwi kudhihirisha kuwa ni pambo lenye dhima kubwa katika ndoa. Mahojiano yetu na makungwi lengwa yanadhihirisha haya.

Shanga zinatumika kuhamasisha mapenzi katika ndoa. Shanga hutazamiwa kwa mawanda mbalimbali na kila wanda likibeba ujumbe wake maalum. Kwa mfano idadi ya shanga anayovalia mke kiunoni inabeba ujumbe mzito kwani avaluapo shanga mbili, ana maana kuwa anahitaji magoli mawili tu katika mchuano na avaluapo tatu au nne vivyo hivyo. Mbali na hayo mke anaweza kuvalia shanga iliyo na bango ndogo lenye maandishi yanayobeba ujumbe mzito wa mapenzi kama vile, ‘nakupenda sana mhabuba.’ Pia rangi

ya shanga anayovalia mke ina ujumbe maalum ulio na uzito wa aina yake. Mathalaan, mke anapovaa shanga nyekundu, atakuwa anamtumia mume ujumbe kuwa siku hiyo yupo kwenye *'traffic lights'* au siku za hedhi.

Maelezo ya kungwi katika dondoo hili kuhusu shanga na rangi zake yanaendana na madai ya Stokes (2016) kuhusu rangi inavyofanikisha mawasiliano bila ya mazungumzo ya sauti. Stokes katika utafiti wake alibainisha kuwa rangi inaweza kuathiri hisia, mtazamo na mawasiliano baina ya watu. Rangi inaweza kuwa na maana maalum katika tamaduni tofauti. Kwa mfano rangi nyekundu inaweza kuchochea hisia za msisimko au hasira au kwa wakati mwingine kuwasilisha ujumbe wa hatari. Hii inashadidia mafunzo ya kungwi katika dondoo hili kuwa mke anapovalia shanga nyekundu atakuwa anawasilisha ujumbe wa hatari yani siku zake za hedhi hivyo kumtahadharisha mume kuhusu kufanya tendo la ndoa. Kwa kifupi, anavyoeleza Harris (2017) shanga zinatumiwa kama nyenzo ya mawasiliano basi mke ataweza kuwasilisha atakacho au anachohisi kwa mumewe kulingana na aina na rangi ya shanga atakayovalia.

2.2.2.5 Matumizi ya Vikuku

Gunter (2021) anasema kuwa vikuku ni mapambo yanayovaliwa kwenye mikono, miguu au sehemu nyingine ya mwili na aghalabu yanayotengenezwa kwa vifaa kama vile mawe, vyuma au vifaa vya kiasili ambayo yana umuhimu maalum wa kitamaduni au kijamii. Ali (2022) kwa upande wake anaeleza kuwa vikuku vinatumiwa kama mapambo ya kuongeza uzuri na mvuto wa mwili vilevile kuwakilisha ahadi na ushirikiano kati ya wanandoa. Zaidi ya hayo, anasema kuwa vikuku huweza kutumiwa kama nyenzo ya kuwasilisha

ujumbe maalum baina ya watu. Katika mahojiano na makungwi lengwa tulibaini kuwa vikuku vina nafasi kubwa katika ndoa kupitia maelezo yafuatayo ya makungwi.

Siku ambayo mke ana jukumu la kumkanda mumewe basi atavalia kikuku cha aina yake kilicho na umbo la duara na kilichotengenezwa kwa plastiki iliyo laini. Fahamu kuwa vikuku vilivyotengenezwa zamani vilikuwa na kengele hivi kwamba mwanamke anapopita sehemu yoyote nyumbani basi atatambulika. Iwapo babamkwe wake atasikia mlio huo wa kengele basi ataondoka njiani au ajibane pembeni ili wasikutane ana kwa ana na mkazamwanawe.

Maelezo haya ya kungwi katika dondoo hili yanaonesha kuwa vikuku vinatumika sana kudhibiti maadili katika jamii ya Waswahili. Mwanamke kuvaa vikuku vyenye kengele kunasaidia kuweka umbali kati yake na babamkwe kwani si vyema wawili hawa kukutana ghafla sehemu za faragha au vichochoroni. Hii ina maana kuwa vikuku ni nyenzo muhimu inayotumika kudumisha amali za kijamii kama vile heshima baina ya mke na babamkwewe. Mbali na kuwa pambo tu la mwili, kikuku kinadhihirika kuwa chenye majukumu makubwa katika jamii ya Waswahili yaani, kama nyenzo ya kudhibiti uhusiano baina ya mke na baba wa mumewe, kukuza na kudumisha amali za kijamii kama vile heshima.

2.2.2.6 Matumizi ya Kinu

Kulingana na Mkapa (2020), kinu ni kifaa cha kijadi kinachotengenezwa kwa mbao na cheye umbo la duara na nafasi katikati ambacho hutumiwa kusaga au kuponda vitu mbalimbali kama vile nafaka au vuingo vya vyakula. Katika jamii nyingi, kinu kina umuhimu mkubwa wa kitamaduni kwani kinahusisha shuguli za familia na jamii kama vile maandalizi ya chakula na sherehe mbalimbali. Miongoni mwa vitu alivyotaja kungwi

lengwa wakati wa mahojiano kuhusu majukumu yao ni kinu. Alisema kuwa, wao hujihami na kinu na mchi wakati wanapomfunza mwanamwali kwa kumweleza namna yakukitumia na maana yake fiche katika ndoa. Alikuwa na haya aliyoeleza kuhusu kinu;

Kinu ni kifaa cha kiasili ambacho mwanamke anafaa awe nacho nyumbani kwake kwa matumizi ainati. Haya ni kama vile kusagia viungo vya vyakula kama vile tangawizi, karafuu mdalasini na vingine au kusagia nafaka na dawa asili. Kuna njia maalun ya kushika mchi wakati wa kusaga au kuponda vitu vilevile kinu nacho huwekwa katika mkao maalum ili kupata matokeo mazuri.

Kauli hii ina jazanda ambayo kungwi ananua mwanamwali wake aielewe kwa muktadha wa mapenzi yake na mumewe. Kungwi anamkumbusha mwanamwali kuwa ndiye aliye na kinu na ana jukumu la kukiweka katika mkao maalum wakati wa 'kusaga' nafaka ili kupata matokeo mema. Ni kutokana na uzingativu wa tasfida ndiposa kungwi anatumia jazanda ya kinu na mchi ili kumwasilishia mwanamwali ujumbe fiche kuhusu uhusiano wake na mumewe.

2.2.3 Namna ya Mke Kuhusiana na Watu Wengine

Mbali na uhusiano baina ya mke na mume, kuna uhusiano mwingine baina ya mke na jamaa za mume, majirani, marafiki na jamii kwa ujumla ambao makungwi hufundisha wanawali. Ili kupata kiini cha mafunzo haya, mtafiti alienda katika mazingira halisi ya kungwi na mwanamwali wake wakati wa mafunzo na kuweza kushiriki darasa hilo. Maelezo ya kungwi ya moja kwa moja wakati wa mafunzo yaliyonakiliwa ni kama yafuatayo;

Ni marufuku kuzitoa siri zako na mumeo kwa watu mwanangu. Usifikiri kuwa kila unayemwambia kuhusu ndoa yako anaifurahia, utaiharibu ndoa yako mwenyewe kwa ulimi wako. Pima kabisa kila unachosema na marafiki zako. Usiseme udhaifu wa mumeo kwa watu. Waheshimu sana wazazi na ndugu wa mumeo. Mwanangu, unakwenda kuolewa, kule unakoenda kuishi kumbuka sio kituo cha redio wala televisheni ukaanze kusambaza habari za ndani kwa umma. Umbeya ni uchafu na sumu kali katika ndoa. Linda kinywa chako unapokuwa na watu wengine maana hao unaodhani ni marafiki watakushauri umuache mumeo ili wamchukue. Iga mfano wa mtungi na kata yake mwanangu.

Dondoo hili lote linasisitiza kuhusu siri. Kuhifadhi siri ya ndoa ndio ngao ya kulinda ndoa. Si vyema kuyasema mapungufu ya mume kwa watu, huko ni kumuumbua. Katika dondoo hili, kungwi anamtaka mwanamwali wake aige mfano wa mtungi na kata yake. Kama ilivyo methali kuwa siri ya mtungi aijuaye kata ndivyo anavyopaswa kuwa mke. Siri zote za mumewe azijue pekee yake wala sio kushirikisha watu wengine.

Mbali na watu wasio wa damu ya mume, dondoo hili linatilia mkazo uzingativu mwingi kwa jamaa za mume, yaani ndugu, wazazi na mashemeji. Pindi tu mke anapofunga pingu za maisha na mume, moja kwa moja anakuwa sehemu ya familia ya mume. Kungwi anamshauri mke kuwaheshimu wazazi pamoja na ndugu za mume ambayo ndiyo ngao ya kuisi vyema katika ndoa yake.

2.2.4 Namna ya Kuzungumza na Mume

Mawasiliano mema kati ya wanandoa ni muhimu sana katika kudumisha uhusiano wa ndoa. Gottman na Silver (2015) wanasema kuwa mawasiliano ni msingi wa kujenga uhusiano dhabiti na wenye furaha. Wanazidi kueleza kuwa mawasiliano yenye ufanisi husaidia wanandoa kuelewa mitazamo na hisia za kila mmoja jambo linalopelekea kupunguka kwa migogoro baina yao. Aidha wanasisitiza kuwa, mausano bora baina ya wanandoa yanafanikisha mambo kadha wa kadha yakiwemo kujua nini cha kusema; wakati gani, mahali gani, na vipi. Kupitia uchunzaji, haya yalijitokeza katika kauli zifuatazo za kungwi lengwa wakati alipokuwa anatoa mafunzo kwa mwanamwali wake.

Mwanangu, mazungumzo yako na mumeo ni muhimu sana na unapaswa kuyamakinikia kwa ustawi wa ndoa yako. Wakati kumezuka tofauti baina yako na mumeo, linda ulimi wako. Ujue ni wakati gani na mahali pepi mwafaka pa kusuluhishia tofauti zenu. Kumbuka kuwa kitanda cha ndoa sio jukwaa la kutatulia tofauti zenu bali ni uga wa mahaba. Katika kuzungumza na mumeo, zingatia sana toni ya mazungumzo yako kwake. Kumbuka kuwa huyo mume wako sio mwanasiasa wa bungeni au mshindani wako wa *debate* za shuleni hivyo, epuka sana hoja za mabishano yasiyo na msingi.

Mambo mbalimbali yanajitokeza katika dondoo hili; kila chumba katika nyumba ya mwanandoa kina jukumu maalum. Kimsingi, sebule ni chumba cha maakuli ila kulingana na wosia wa kungwi katika dondoo hili, kinaweza kuwa sehemu ya kuzungumzia na kutatulia migogoro baina ya wanandoa. Aidha, chumba cha kulala kina jukumu moja kuu la kuwa eneo la mahaba baina ya wanandoa wala sio sehemu ya kusuluhishia migogoro. Haya yanadhihirisha kuwa kitanda cha ndoa kina siri kubwa na ni jukumu la wanandoa kudumisha hili.

Jambo jingine linalojitokeza katika dondoo hili ni kuhusu toni ya mazungumzo. Toni ina athari kubwa katika mazungumzo baina ya wanandoa. Utafiti unaonyesha kuwa, jinsi wanandoa wanavyozungumza ikiwemo sauti, lugha ya mwili, uteuzi wa maneno miongoni mwa mengine, unaweza kuathiri hisia zao na uwezo wao wa kutatua migogoro (Gottman, 2016). Mtafiti huyu wa maswala ya ndoa anasema kuwa matumizi ya toni ya upole na utulivu husaidia kuboresha mazungumzo huku toni ya ukali na yenye hasira inaweza kuanzisha migogoro. Haya yanaenda sambamba na wosia wa kungwi katika dondoo hili kwa mwanamwali wake anaposema, *“kumbuka kuwa huyo mume unayeenda kuolewa naye sio mwanasiasa wala mshindani wako katika debate za shuleni.”* Kauli hii ni wosia kwa mwanamwali kuepuka ushindani na mumewe na pia asitumie toni ya juu kwa mumewe kana kwamba wapo bungeni au mijadala za shule.

2.2.5 Uzingativu wa Usafi

Katika kuidhibiti na kuidumisha ndoa mke anashauriwa kuliweka swala la usafi katika mstari wa mbele. Usafi anaorejelewa hapa ni wa vitengo vyote vikiwemo usafi wa mwili na wa mazingira. Kwa kuwahoji makungwi lengwa kuhusu dhima yao, walitilia mkazo kuwafundisha wari wa kike kuhusu usafi. Kwa usafi wa mazingira, kungwi aliyehojiwa alisema yafuatayo wanayowaarifu wari wao wakati wa mafunzo.

Mume anaweza kutoka kazini na kuamua kurejea nyumbani na rafiki zake. Itakuwa aibu kubwa anapoingia kwa nyumba anakutana na nguo za watoto chini mlangoni huku sufuria zimezagaa juu ya meza, nyumba nayo haijadekiwa, vitambaa kwenye makochi havijatandikwa ilhali mke ameketi tu bila wasiwasi wowote. Huu ni usungo mkubwa.

Dondoo hili linadhihirisha kuwa, jukumu kubwa la mke katika ndoa ni kuhakikisha usafi wa mazingira anamokaa umedumishwa. Usafi wa ndani ya nyumba unahusisha mpangilio mzuri wa vitu vilivyomo ndani ya nyumba, kupiga deki na kusafisha vyote vilivyomo ndani ya nyumba. Hili linamvutia mume na kumpa hamu ya kurejea kwake baada ya kazi kwani ni mahali penye mvuto wa aina yake. Wakati wowote anapoamua kurejea kwake na rafiki zake, ana uhakika wa kuipata nyumba ikiwa nadhifu.

Kitengo kingine alichokipa kipaumbele kungwi katika mafunzo yake kuhusu usafi ni kuhusiana na usafi wa mwili. Hapa, makungwi hawa walisema kuwa wao huwafundisha wanawali kuhusu usafi wakati wa hedhi kwani kipindi hiki huhitaji uzingativu wa usafi wa hali ya juu. Kando na wakati wa hedhi, usafi wa mwili wa mara kwa mara ulisisitizwa.

Mahojiano na kungwi lengwa yaliibua yafuatayo;

Mke anapaswa kuzingatia usafi wa mwili ili kumvutia mumewe kila mara. Mara nyingi wanawake wengi baada ya kujifungua hata mtoto mmoja, hujisahau na kuacha kujinadhifisha kabisa. Baada ya kumshughulikia mtoto kama kumlisha au kumlea, aoge mara kwa mara na kubadilisha mavazi yake ili awe na mvuto kwa mumewe. Anapaswa kuonekana mpya kila siku machoni mwa mumewe.

Mawaidha haya ya kungwi kwa mwanamwali yanamkumbusha mke kuwa yeye ni pambo kwa mumewe hivyo, anapaswa kupendeza kila wakati. Huenda anapolisha mtoto akajichafua kwa namna nyingi kama mtoto kumwendea haja au kumchafua na chakula chake. Kwa vyovyote vile, hawezi kuepuka jukumu la kumhudumia mtoto bali uzingatuvu wa usafi unapaswa kuwa mstari wa mbele. Anapaswa kuoga na kubadilisha mavazi yake ili awe na mvuto kwa mumewe. Iwapo ni mwenye kupenda manukato, ajirashie pamoja na nyumba yake ili kuleta harufu ya mvuto.

2.2.6 Adhabu kwa Wanawali Wasiotii

Kungwi wana jukumu lingine la kuwaadhibu wanawali wasiotii mafunzo wanayopewa. Baada ya kumpokeza mwanmwali mafunzo ya unyagoni kuhusu matumizi ya vifaa mbalimbali katika ndoa na maana yake, majukumu ya mke katika ndoa na mambo anayotarajiwa kuyaepuka basi mwanamwali anapaswa kuyazingatia. Asipozingatia mafunzo haya basi ataadhibiwa na kungwi wake aliyemfundisha. Ili kupata jukumu hili la kungwi mahojiano ya kina yalifanyika na kungwi lengwa akatoa maelezo haya;

Tunapofunza mwari wetu tunatarajia awe mtiifu kwa mafunzo yote. Anapoenda kinyume kwa njia yoyote ile kwa mfano kusema siri za ndoa yao kwa watu, kutomhudumia mumewe vyema au kutotekeleza majukumu yake yote kwa ujumla basi hua tunamwadhibu. Adhabu yetu ni kumuita kokoni na kumpiga kwa kututia aibu kwa kutozingatia mafunzo yetu. Mwanamwali kama huyu asiyesikia mafunzo huitwa ‘mwalibewa’ yaani asiyesikia. Baada ya kumpiga huwa tunamfunza tena.

Dondoo hili linafundisha kuhusu utiifu wa mafunzo. Makungwi wanapowafundisha wanawali huwasisitizia umakini na utiifu. Jambo jingine linalojitokeza katika dondoo hili ni kuwa, kungwi wana jukumu la kuwafuatilia wanawali ambao wanawafundisha wanapoingia katika ndoa zao. Lengo hili ni kudhibitisha iwapo wari hawa wanayazingatia mafunzo waliyowapa au la. Iwapo mwanamwali atafeli katika ndoa yake na kuishia kupewa talaka basi wa kulaumiwa ni somo wake kwa kutomfundisha vyema. Hii ndio sababu makungwi huwaadhibu wari wasio watiifu ili wasiwapake tope.

2.3 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili ambapo historia fupi kuhusu utamaduni wa Waswahili imetolewa. Katika sehemu hii, kiini cha utamaduni wa unyago unaohusisha mafunzo ya kungwi kwa wanawali kimeangaziwa. Aidha, mafunzo ya kungwi kwa wanawari yameshughulikiwa ambapo yale makuu yaliojadiliwa kwa kina ni namna ya kumhudumia mume, mafunzo ya vifaa na maana yake, namna ya mke kuzungumza na mume pamoja na watu wengine, na mafunzo ya usafi. Sura inayofuata inatoa mjadala kuhusu maudhui ya ukungwi yanazojitokeza katika nyimbo teule za taarab.

SURA YA TATU

MAUDHUI YA UKUNGWI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB

3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Chimbuko na maendeleo ya nyimbo za taarab limetolewa ili kudhihirisha ufungamano wa utamaduni wa mafunzo ya ukungwi na nyimbo za taarab.

3.1 Asili ya Nyimbo za Taarab

Taarab ina mizizi ya muziki wa Kiarabu hasa mtindo wa mzunguko unaojulikana kama *oud*, *qanun* na *darbuka* lakini pia inajumuisha athari za muziki wa Kiswahili na wa Kibantu (Kamwendo, 2009). Msomi huyu anaeleza kuwa asili ya nyimbo za taarab ni mchakato wa kihistoria na kitamaduni unaohusisha mchanganyiko wa muziki wa Kiarabu na Kiafrika. Kulingana na Kamwendo, muziki wa taarab ulianza mwishoni mwa karne ya 19 katika Pwani ya Afrika Mashariki hususan miji ya Zanzibar, Mombasa na Dar es Salaam.

Mwanaisimu na mtaalam wa muziki wa taarab Khamis (2012) anasema kuwa, muziki wa taraab uliletwa na Waarabu kutoka bara la Arabia kupitia bandari za Zanzibar na za Pwani ya Afrika Mashariki kwa ujumla ambapo meli za biashara zilifika. Mtaalamu huyu anazidi kueleza kuwa, taarab ilikua na kuenea Zanzibar maeneo ya Pwani ya Afrika mashariki baada ya Waarabu kuanzisha biashara ya utumwa na kuleta tamaduni zao zikiwemo muziki wa Kiarabu vilevile ala za kiasili za muziki wa taarab kama vile *oud*,

darbuka na *aanun*. Sheto (2012) kwa upande wake naye anasema kuwa, mbeleni taarab ilifanyika kama muziki wa sherehe na hafla kubwa za kifalme ambapo ulihusisha mchanganyiko wa mashairi ya Kiswahili na midundo ya Kiarabu. Licha ya taarab kuwa na mizizi yake Uarabuni, Sumra (2010) anasema kuwa, muziki huu wa taarab unahusiana na utamaduni wa Waswahili ambapo taarab inajumuisha mchanganyiko wa mashairi ya Kiswahili ambayo ilitoa fursa kwa watunzi wa mashairi kuandika mashairi yenye maudhui ya mapenzi, huzuni siasa miongoni mwa mengine. Hii ilileta mvuto kwa wengi na kuifanya taarab kuwa muziki wa lugha Kiswahili.

Kiswahili ni lugha ya kiasili ya Pwani ya Afrika mashariki na sasa kinatumika kama lugha ya kuwasilishia maudhui ya muziki wa taarab (Abulaziz, 2007). Kulingana naye, taarab ni moja wa vyombo vya kuhamasisha na kueneza lugha ya Kiswahili. Aidha, anazidi kueleza kuwa, mashairi ya taarab aghalabu huwasilisha hadithi za kihistoria, mapenzi na masuala ya kijamii kupitia lugha ya Kiswahili. Hii imewezesha jamii ya Waswahili kuelewa na kuhifadhi urithi wao wa kihistoria na wa kiutamaduni. Hii inadhihirisha kuwa taarab ni nyenzo muhimu ya kuenzi na kuhamasisha utamaduni wa Waswahili.

Sumra (2010) anaeleza kuwa muziki wa taarab ulijengwa katika utamaduni wa Waswahili hususan katika muktadha wa sherehe za ndoa ambapo taarab ilitumiwa kuhamasisha furaha na mshikamano baina ya watu. Maelezo ya Khamis (2012) vilevile yanaoana na ya Sumra (2010) anaposema kuwa maudhui ya taarab yana uhusiano mkubwa na maadili ya utamaduni wa Waswahili. Anazidi kueleza kuwa taarab inaeleza maadili ya familia

kama vile umuhimu wa kuzingatia haki na usawa katika jamii na wosia wa masuala ya ndoa wa ujumla.

Maoni ya wasomi hawa yanadhihirisha kuwa maudhui katika nyimbo za taarab yamefungamana na utamaduni wa Waswahili. Utamaduni wa Waswahili unaohusisha mila na desturi za mafunzo ya unyagani ni mmojawapo wa utamaduni unaoimbwa kwa sana katika nyimbo za taarab.

3.2 Maudhui ya Ukungwi katika Nyimbo Teule za Taarab

Sehemu iliyotangulia imeonyesha uhusiano uliopo baina ya nyimbo za taarab na utamaduni wa Waswahili. Aidha, Waswahili wanahusishwa na utamaduni wa mila na desturi za unyago ambazo zinahusisha mafunzo ya masuala ya ndoa. Waimbaji mbalimbali wa nyimbo za taarab huchota malighafi yao katika jamii inayowazunguka hivyo kuishia kuimba masuala ya utamaduni wao wa unyago. Sehemu hii imedhihirisha namna nyimbo teule za taarab zinavyoibua maudhui ya ukungwi. Mchakato wa uchanganuzi wa masuala haya umeongozwa na nadharia ya Simiotiki. Pierce (1977) ameeleza Simiotiki kama nadharia inayozungumzia uashiraji wa vipashio vya lugha kwa kujaribu kuonyesha namna kazi za kifasihi hupata viashiriwa (maana) yake katika muktadha wa kijamii. Wanasimiotiki wanaeleza kuwa maana katika ishara za kifasihi inaweza kubainika kutokana na mfumo wa ishara zingine, muktadha wa kijamii, njia ya kimafumbo au ile ya moja kwa moja. Kutokana na mhimili huu, tunabaini namna maana inayojitokeza katika nyimbo teule za taarab imefungamana na utamaduni wa Waswahili wa mafunzo ya ndoa.

3.3 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa *Maji ya Uvuguvugu wa Wachonga*

Vinyago

Wimbo huu umeimbwa na kundi la wanawake watatu ambao wanamlenga mwanamke aliye katika ndoa na kumpa mafunzo ya kile anachostahili kukifanya ndoani mwake. Maudhui ya ukungwi yanadhihirika katika wimbo wa *Maji ya Uvuguvugu* kwa njia anuwai kutokana na jinsi waimbaji wamewasilisha ujumbe wao. Ujumbe umewasilishwa kwa njia ya moja kwa moja na ya njia ya kimapumbo kutokana na uzito wa ujumbe uliyomo. Kifungu kifuatacho cha wimbo huu kinaibua maudhui ya ukungwi yanayohusiana na namna mke anavyostahili kujiendesha katika ndoa yake. Mwimbaji wa kwanza anaimba;

Mwanaume tunza, yapasa kumtunza
Mambo usiyabanange, usije kuyavurunda

Mstari wa kwanza katika kifungu hiki unatoa ujumbe kwa njia ya moja kwa moja inayoeleweka kwa urahisi. Njia hii ambayo Peirce (1998) anaieleza kuhusu namna kazi za kifasihi zinavyowasilisha ujumbe kwa kutumia njia iliyo dhahiri na ya kueleweka. Hapa, mwanmwali anayeingia ndoani anashauriwa kumtunza mumewe kwa hali zote ili kulidumisha penzi baina yao. Anamkumbusha kuwa ni jukumu lake ambalo anapaswa kulitekeleza kama mke. Aidha, msanii anatumia neno ‘kubananga’ na ‘kuvurunda’ kuwasilisha ujumbe wa ukungwi kwa mwanmwali. Kulingana na Tenge (2019) kubannga mambo ni dhana inayohusiana na hali ya kufanya mambo kwa njia pevu isiyojali athari za ustawi wa jumla. Hii ina maana ya kutatua matatizo kwa haraka na kwa uwazi bila kujali athari zinazoweza kufuata. Kutokana na haya, ujumbe unaojitokeza kwa muktasari

huu katika kifungu hiki ni kuwa, mke hapaswi kuyaweka wazi mambo yake ya ndoa akitarajia kuwa ndio njia ya kupata suluhisho la yoyote yanayomkumba. Anashauriwa kuwa, kuyaweka wazi kwa njia ambayo masuala ya ndani ya ndoa sio suluhu bali ni kuyaharibu hata zaidi. Hii ndiyo maana anatahadharishwa kuwa asiyaweke mambo yake ya ndoa wazi aisje akayavurunda.

Aidha kulingana na wanasimiotiki, tafsiri ya ishara hufanyika kwa mujibu wa kijamii na kitamaduni. Ishara kwa mujibu wa Saussure (1983) ni dhana au majina yanayorejelea vitu halisi. Hivyo, kutokana na maelezo ya Wanasimiotiki, ishara fulani hupata tafsiri mwafaka zinapohusishwa na jamii maalum. Zipo ishara ambazo zimetumika katika wimbo huu ambazo tafsiri yake katika muktadha wa jamii ya Waswahili inaibua maudhui ya ukungwi. Kifungu kifuatacho kutoka wimbo wa *Maji ya Uvuguyvugu* kinadhihirisha haya.

Usiwe kama msungu, mwanamwali wewe umefundwa
 Hata *special* pia yaweza kuwa mtumba
 Mume usije mfuja, siri za ndani zikavuja
 Bibi mtunze mumeo kuna kunguru wa Unguja

Kutokana na mstari wa kwanza, msanii anamshauri mwanamwali asiwe kama msungu kwani ameshapokea mafunzo ya ukungwi. Neno (ishara) ‘msungu’ linapotafsiriwa katika muktadha wa utamaduni wa jamii ya Waswahili, lina maana ya mwanamwali anayekosa kuzingatia mafunzo anayopokezwa na Kungwi wake (Khamis, 2017). Maelezo ya mataalamu huyu wa masuala ya unyago, yanatuongoza kubaini kuwa, mwanamwali anapaswa kutilia maanani mafunzo anayopokea kutoka kwa makungwi wake. Halikadhalika, ‘mtumba’ limetumika kuashiria maana maalum yanayohusiana na

mafunzo ya unyago yanayotolewa na makungwi. Msanii huyu anasema; *hata special pia yaweza kuwa mtumba* akiwa amefumbata maana yake. Mwangangi, (2018) amefanya utafiti kuhusu mitumba na kutokana na utafiti wake, dhana mtumba imefasiriwa kama vitu visivyo vipya vinavyouzwa kwa bei ya chini mno. Hii ina maana kuwa kuna wakati vitu hivi vya mtumba vilikuwa vipya na vyenye hadhi ya juu lakini baada ya kutumika sana thamani yake ikapungua. Kulingana na wimbo huu, msanii anamkumbusha mwanamwali kuwa, aingiapo katika ndoa anakuwa na thamani ya juu na ni katika nafasi hii anamrejelea kama *special*. Kadri muda unavyozidi kusonga, hadhi yake inashuka na kuwa kama mtumba. Hivyo basi anashauriwa kuzingatia sana mafunzo aliyopokezwa na somo wake ili kudumisha thamani yake.

Mstari wa mwisho katika kifungu hicho unatoa ushauri kwa mwanamwali kwa njia ya kimafumbo. Msanii anasema; *bibi mtunze mumeo, kuna kunguru wa Unguja* kuashiria maana fiche kwa wenye njama mbaya kwa ndoa husika. Rajab F.H (2006) anaeleza kuwa kunguru ni aina ya ndege mwenye mazoea ya kula vitu vilivyoachwa ovyo kama mizoga. Binadamu wenye mazoea ya kukula vilivyoachwa wanaweza kulinganishwa na kunguru. Hii ndiyo maana msanii anamshauri mwanamwali kumtunza mumewe dhidi ya wanawake wa Unguja (*kunguru wa Unguja*) wanaoweza kumnyakua mumewe.

Peirce (1998) anaelezea msimbo wa kisemantiki unaofafanua maana inayobebwa na ishara ambayo ni ya moja kwa moja na inaeleweka kwa haraka. Zipo ishara katika matini za kifasihi zinazotoa maana ya moja kwa moja ambayo inaeleweka kwa urahisi. Kifungu

kifuatacho kinabeba ishara zinazoashiria maudhui ya ukungwi kwa njia ya moja kwa moja.

Maji ya uvuguvugu, mtengee aoge
 Mume hataki vurugu, anataka utulivu
 Mpake poda mumeo, usijempaka jivu
 Raha ya penzi linoge, mwanamwali usiwe na wivu
 Kamtunze mume wako, wala usiwe na wivu

Ujumbe katika dondoo hili umewasilishwa kwa njia ya moja kwa moja kuelezea maudhui ya ukungwi. Mwanamwali anashauriwa kumtengea mumewe maji ya uvuguvugu kila anapohitaji kuoga. Anapaswa kuhakikisha kuwa maji anayomtengea kuoga yapo katika hali nzuri na yasiwe baridi mno wala moto sana. Pia, anashauri kuepuka vurugu ya aina yoyote kwani kila wakati mume hupenda amani ya moyo kila mara. Anashauriwa kuwa utulivu katika ndoa hupalilia mapenzi baina ya wanandoa hivi kwamba iwapo kuna jambo la kutatuliwa basi kunayo mazingira bora ya kulitatulia.

Katika dondoo hili pia msanii amezungumzia suala la kumpaka mume poda wala sio jivu. Kauli hii imetumika kijazanda kuashiria uwazi ambao mwanamke anapaswa kuwa nao wala sio unafiki. Kumpaka mume jivu ni jazanda inayoashiria kumtendea vitendo visivyofaa wakati anapohitaji huduma kutoka kwake. Hii ina maana kuwa mke anashauriwa kuwa mkweli kwa mumewe na kumtendea matendo yanayofaa. Hii inajumuisha masuala ya kumtunza vyema na kuepukana na wivu ili kudumisha mapenzi baina yao.

3.4 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa *Bi. Arusi wa AT*

Mwimbaji wa wimbo huu ametumia njia mbalimbali kuwasilisha maudhui ya ukungwi ikiwemo jazanda, kejeli kinaya miongoni mwa njia zingine. Wasanii wengi hutumia mbinu za kisanaa kufumbata ujumbe muhimu katika kazi zao za kifasihi. Kejeli imetumika kuwasilisha maudhui ya ukungwi katika wimbo huu. Kulingana na Gikandi (2000), kejeli ni mbinu ya kifasihi inayotumika kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kudhihaki au kudunisha tabia hasi kwa kutumia aghalabu lugha yenye mifano. Katika kazi za kifasihi kejeli hutumika kuweka dhahiri udhalimu wa kijamii, kimazingira au kimaadili kwa njia ambayo inavutia msomaji kutafakari kwa undani na kujifunza kutoka kwa udhaifu unaodhihirishwa. Katika wimbo huu, msanii ametumia viashiria vyenye maana ya mafunzo ya ndoa yanayotolewa na makungwi. Msanii wa wimbo huu amemlenga Bi. Harusi kama hadhira yake na kumfikishia ujumbe wenye mafunzo ya ndoa kwa njia ya kejeli. Haya yanadhihirika kupitia kifungu kifuatacho anaposema;

Umetaniwa kidogo unatoa matapishi
Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi
We jifanye mjuaji kapike wali mbichi
Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi

Kifungu hiki kinaonesha kuwa msanii anatoa mafunzo kwa Bi. Harusi kwa njia ya kukejeli tabia hasi kwa mke katika ndoa. Anakashifiwa kwa tabia ya kutoa matusi anapofanyiwa utani. Msanii anamkejeli anapomwambia kuwa anapotaniwa tu kidogo anatoa matapishi. Matapishi ni uchafu wa chakula unaotolewa kupitia kinywani mwa mtu hivyo hapa limetumiwa kuonesha maneno machafu ya kumtoka kinywani mwa mke. Katika kejeli hii vilevile anatoa mafunzo kwake ya kuzoea kutaniana na watu vilevile

kukubali kutaniwa katika ndoa kwani utani ni sehemu ya mahusiano ya watu na vilevile unachangamsha mahusiano baina ya watu.

Mbali na kejeli ya namna hiyo kwa mwanamwali katika kifungu hiki, mke anataniwa kwa tabia yake ya ujuaji kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kwake. Utani ni mbinu mojawapo ya kuwasilisha ujumbe wa kazi za kifasihi. Utani huzungumzia tabia fulani kwa wepesi au kwa kupunguza ukali wa maneno. Katika mstari wa tatu wa kifungu hiki, msanii anasema; *we jifanye mjuaji kapike wali mbichi*. Katika kumtania mke kwa tabia yake ya ujuaji, msanii anawasilisha ujumbe kwake wenye mafunzo mazito kuwa ni vyema kuuliza kuelekezwa kwa jambo asilolijua ili kujiepushia balaa. Anajaribu kudhihirisha kuwa kuuliza jambo usilolifahamu vyema sio ujinga bali unaepusha aibu inayotokana na kuharibu jambo lenyewe. Kulingana na msanii pia, mapishi bora ni sifa muhimu kwa mke ndiposa anamsisitizia mwanamwali huyu ubora wa kuuliza namna ya kupika wali kuliko kujiletea aibu anapoupika mbichi.

Pia tabia hasi ya mwanamwali inakejeliwa kwa madhumuni ya kutoa mafunzo kuhusu namna ya kujiendesha katika ndoa. Msanii anamkejeli mwanamwali ambaye amemuita kwa jina Wanja kwa kuwa na tabia isiyostahili kwa mkwewe. Mwanamwali huyu anakashifiwa kwa kutoa maneno ya matusi kwa mkwewe. Anasema katika mstari ufuatao;

Kina mama mabibi na mababu, nawashika masikio
Hawa wari wa sasa wana taabu, waozeshwe mbiombio
Wanja ana tabia mbaya anamsema, mkwewe eti kwamaba ana chawa

Kutokana na upotovu wa maadili miongoni mwa wanawali, kina mama, mabibi na mababu wanashauriwa kuwaozesha mabinti wao haraka. Kwa kutozingatia mafunzo wanayopewa na somo wao kuhusu namna ya kuhusiana na wakwe zao wanaonekana waliopotoka kimaadili. Mhusika Wanja kumsema mkwewe vibaya kuwa ana chawa ni tabia ya kukashifiwa isiyostahili kwa mwanamwali yeyote aliyepokezwa mafunzo na somo wake. Hii ndio maana wanawali wanashauriwa kuwa na uhusiano mwema na wakwe zao wanapokuwa katika ndoa.

Mbali na wosia wa uhusiano mwema, msanii anazidi kumshauri mwanamwali kudumisha mlahaka mwema na wakwe zake kwani wana nafasi kubwa sana katika ufanisi wa ndoa yao. Msanii anampa mwanamwali ngao ya kudumisha mlahaka mwema kati yake na mwanamwali ambayo ni furaha na uchangamfu. Anasema kuwa, ili kuishi vyema na mke wakwe wake, avae uso wa furaha, na uchangamfu anapotagusana naye. Haya yanajitokeza katika kifungu kifuatacho;

Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi
 Manyakanga mko wapi leo mje muamue kesi
 Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi
 Mtizameni mkwe wenu kwa bashasha na ucheshi

Kutokana na kifungu hicho, mwanamwali aingiapo katika ndoa, anatakiwa kuwa na uhusiano mwema na wakwe zake. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa uchangamfu na furaha huleta ufanisi wa uhusiano kati ya wahusika (Mehrabian, 1971). Hali hii inasaidia kujenga mazingira ya ushirikiano na maelewano baina ya wahusika. Aidha, furaha katika mazungumzo inaweza kuwa kichocheo cha kubadilisha mtazamo wa mtu juu ya mwingine au juu ya suala fulani. Kutokana na haya, ni dhahiri kuwa, mke anapomtazama

mama mkwewe kwa bashasha na ucheshi kila wanapotagusana anajenga uhusiano mwema baina yake na wakwe zake hivyo kuepusha ugomvi.

Barthes (1994) anazungumzia msimbo wa kimatukio ambao unahusu utokeaji wa matukio au kisa chenye maana fiche. Anazidi kufafanua kuwa matukio mengine hufumbata ujumbe wake kulingana na lugha inayotumika ambayo huweza kuwa fiche isiyo dhahiri. Katika wimbo huu, msanii anaibua muktadha wa tukio la kisherehe ambapo ni katika sherehe hii ndipo mwanamwali anafanya kitendo cha kuajabiwa. Msaanii anasema;

Mimi na wewe tusipeane lawama
 Umealikwa ya nini ukimbie na nyama
 Mimi na wewe tusipeane lawama
 Umealikwa ya nini ukimbie na nyama

Tukio linaloibushwa na msanii katika kifungu hiki ni la kualikwa katika sherehe ambapo katika sherehe hii ndipo mwanamwali aliyealikwa anakimbia na nyama. Sherehe ni mahali ambapo pana watu wengi hivyo mtu anatarajiwa kutunza heshima yake kwa kuepuka kutenda matendo ya kumtia aibu. Mwanamwali ambaye anarejelewa katika kifungu hiki anatenda matendo ya kuajabiwa ya kukimbia na nyama anapoalikwa karamuni. Kukimbia na nyama imetumika kubainisha maana ya kujiaibisha mbele ya watu unapoalikwa karamuni. Haya ni mafunzo kwa wanawali ya kuwa na ustaarabu na kudumisha heshima yao wanapokuwa katika kundi la watu.

Msimbo wa kisemantiki unaeleza kuhusu maana iliyofichika katika matini au mazungumzo na inatokana na uhusiano kati ya ishara na vitu au dhana zinazowakilishwa na ishara hizo. Mbali na maana ya kimsingi ambazo zinaashiriwa na kauli za kisanaa,

zipo maana za ziada ambazo kauli hizo zinaibusha. Ishara inapata maana ya ziada kutoka na muktadha ambao imetumika. Muktadha huu waweza kuwa wa kiutamaduni au wa kimatini yenyewe. Msanii katika kifungu hiki cha wimbo ametumia mtindo huu kuwasilisha maana kwa hadhira yake lengwa. Haya yanajitokeza katika kifungu kifuatacho.

Eh mama lawama kanipa shubiri kaniambia nyama
 Eh mama lawama kanipa shubiri kaniambia nyama
 Dada yake Bi. Harusi yuko wapi aje hapa
 Nimekuja na mzigo leo nataka kumpa

Shubiri katika kifungu hiki ni ishara iliyotumika kudhihirisha maana yake ya kimsingi na ile ya ziada kutokana na muktadha wa kimatini ambao ishara hii imejitokeza. Kimsingi, shubiri ni kitu kichungu sana ila ishara hii inapotumika katika maana hii inaibua maana pana. Katika kifungu hiki msanii anaonekana kulalamikia kitendo anachotendewa na Bi. Harusi hadi anataka kumpata dada yake kumfahamisha kitendo kiovu anachotendewa na Bi. Harusi. Amempikia nyama vibaya ambayo ni chungu mithili ya shubiri jambo linalomgadhambisha sana. Haya yanaashiria kuwa mapishi mazuri ni nguzo muhimu kwa mwanamke kwani apikapo vibaya, watu wa familia yake kama madada wanaweza kujuzwa kuhusu hili au hata akarejeshwa kwao.

3.5 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa *Ndoa* wa Aslay na Hadija Kopa

Wanasimiotiki wanaeleza namna ishara zinavyobeba maana inayoeleweka kwa haraka na kwa njia ya moja kwa moja. Peirce (1998) anatumia mfano wa rangi nyekundu inayoweza kubeba maana ya upendo au hatari. Vivyo hivyo, wakati mwingine, ishara zinazotumika katika matini au usemi wa kifasihi zinabeba maana inayoeleweka kwa urahisi. Haya

yanajitokeza katikaHebu kifungu kifuatacho kutoka wimbo wa *Ndoa* ulioimbwa na Aslay akimshirikisha Hadija Kopa.

Mwanangu uchechemee
 Ulofundwa usiyaseme kwa watu
 Maneno umumunye
 Ya chumbani usiwape faida watu

Katika kifungu hiki mwanamwali anashauriwa kutoparamia mambo kwa pupa bali awe makini. Mwimbaji anaposema mwanangu uchechemee ana maana ya kuyaendea mambo kwa umakini mkubwa wala sio kwa pupa. Kutembea kwa kuchechemea ni ishara ya umakini katika kutekeleza mambo. Pia anashauriwa kutoyasema kwa watu yale aliyofundishwa (aliyofundwa) unyagoni na somo wake. Kauli hii ina maana kuwa mafunzo anayopokezwa mwanmwali yana usiri mkubwa na hayapaswi kusemwa ovyoovy kwa watu. Haya pia yamekaririwa na Khamis (2015) katika utafiti wake unaohusiana na mafunzo kwa mwanamke. Mtafiti huyu anasema kuwa, mwanamwali kuyaweka siri mafunzo aliyopokea kutoka kwa somo wake husaidia kuhifadhi hadhi na heshima yake kwani katika kuyasema anaweza kujikuta akijitia aibu kwa kusema mambo yake ya siri. Vilevile, usiri kuhusu mafunzo ya ndoa unalenga kuhifadhi mila na desturi zinazohusiana na masuala ya unyagoni. Khamis (2015) anaeleza kuwa, yapo mafunzo mengi ambayo yanahusu jinsia ya kike tu ambayo yanahusiana na namna ya kuitunza ndoa yao na anapoyasema kwa watu wa kiume, humtia mwanamwali husika aibu. Ni kutokana na haya ndipo msanii anasema ya *chumbani usiwape faida watu*. Kauli hii ina maana kuwa mke hastahili kufichua siri za chumbani zinazohusu mambo yake na mumewe. Haya yanawahusu wao wawili na iwapo ni ya kutatuliwa basi wasihusishe mtu

mwingine. Mwanamwali anapoyasema haya ya chumbani kwa watu anatia doa katika ndoa yake. Hii ndiyo maana msanii katika wimbo huu analitilia mkazo hili anaposema;

Ndoa usiitie doa
Ukiitia ndoa doa utanita haya

Doa katika kiitikio hiki linatokana na hali ya mke kuyaweka hadharani masuala ya chumbani na yote aliyofundishwa mwanamwali. Mke anapoyasema ya chumbani kwa watu, hujikuta akiusema upungufu au udhaifu wa mumewe ambapo ni kumpaka tope hivyo kumtia haya somo wake aliyemfundisha usiri.

Jambo jingine ambalo msanii analiangazia katika kutoa mafunzo ya ukungwi kwa mwanamwali ni matumizi ya simu. Msanii anazungumzia jamii ya kisasa ambayo imetawaliwa na usasa wa matumizi ya teknolojia mpya hususan simu na mitandao. Mitandao za kijamii kama vile *Whatsapp* zisipotumiwa vyema basi zitaathiri ndoa kwa njia hasi. Msanii wa wimbo huu anaelezea hili anaposema;

Wanawake wa kisasa mnajifanya mna *Whatsapp*
Hamna muda wa kuwashughulikia waume zenu
Wacha mchezo wenzio *watakuwhatsapp* mume

Katika kifungu hiki, kuna mambo mawili yanayojitokeza waziwazi, kwanza, wanawake katika ndoa wametekwa na mtandao wa *Whatsapp* kiasi kwamba wanatumia muda wao mwingi hapo na kukosa kumtengea mume muda. Hii inakuwa njia ya kutia doa ndoa hivyo chanzo cha kuvurugika kwake. Matumizi ya mtandao wa *Whatsapp* kupitiliza yanamfanya mke kukosa kutekeleza majukumu yake aliyofundishwa na somo wake kama vile kumtayarishia mume chakula kwa wakati kumtayarishia maji ya kuoga miongoni mwa majukumu mengine. Jambo jingine linalojitokeza katika dondoo hili ni kuwa mitandao za kijamii kama *Whatsapp* wanazotumia wanawake wa kisasa walioko ndoani

ndizo huwapokonya waume zao. Haya yanadhihirika kutokana na kauli ya wasanii katika wimbo huu; *wacha mchezo wenzio watakuwhatsapp mume*. Kauli hii ina maana kuwa iwapo mke atakosa muda na mumewe na kuutumia muda wake mwingi kwenye mtandao *Whatsapp*, basi ni kupitia tu hiyo *Whatsapp* ndipo mumewe atapata mwanamke mwingine wa kumliwaza au kumtengea muda. Wanapokosa penzi kwa wake zao basi wanalitafuta kwingine kwa wanawake wengine.

Msanii anatoa ushauri wa moja kwa mwanamwali kuhusu namna anapaswa kuhusiana na mumewe, marafiki pamoja na wakwe zake. Msanii huyu anamshauri mwanamwali kudumisha amani katika ndoa kwa kuzungumza vyema na mumewe kila wanaposhiriki jambo. Anasema;

Usipende kugombana na mume wako
Hata kama kuna kitu kimekukwaza
Rudi vikizidi vituko, ama nyumbani kwako hujafukuzwa

Katika dondoo hili, ujumbe unajitokeza wazi wazi kuwa, mke anapaswa kuwa makini katika hatua anazochukua. Kila kunapozuka jambo katika ndoa. Mke anashauriwa kuepuka kugombana na mumewe kwa, vyovyote vile. Aidha, maji yanapozidi unga, kunapozuka migogoro ya mara kwa mara pamoja na zogo asiyoweza kuidhibiti, basi anashauriwa kurudi nyumbani kwao. Msanii anajaribu kumtayarisha mwanamwali kuwa hakuna ndoa inayokosa migogoro ila, hali hii inapokithiri zaidi ni heri kurudi kwao kuliko kujiletea madhara kama vile kujeruhiwa, au hata kuuwawa. Hii inadhihirisha kuwa, hakuna mwiko wowote wa kijamii unaomzuia mke kurudi nyumbani kwao anapofunga pingu za maisha.

Ushauri mwingine unaotolewa na msanii huyu unahusu uhusiano wa mke na watu wengine kama vile marafiki vilevile wakweze. Anamtolea ushauri wa moja kwa moja kuwa anapaswa kumakinika na watu anaohusiana nao kwani wanaweza kuiharibu ndoa yake. Anamuonya kwa hili anaposama;

Mashoga wataiharibu ndoa yako
Watakupinduapindua watamteka mume wako
Jitahidi uwaheshimu wakwe zako
Hizo ndizo nguzo za kutunza ndoa yako

Hapa, msanii anamuonya mwanmwali dhidi ya kuwashirikisha marafiki zake wa kike katika ndoa yake. Anatakiwa kutowahusisha kwa namna yoyote ile, kwenda kuwalalamikia kuhusu matatizo yanayomkumba katika ndoa, kuwaomba ushauri kuhusu ndoa yake au kuwahusisha kwa masuala yake. Hulka ya marafiki wengi ni kumpotosha kwa ushauri kwa lengo la kumteka mume wake. Anamkumbusha mwanamwali kuwa nguzo kuu ya kuitunza ndoa yake ni heshima.

3.6 Maudhui ya Ukungwi katika Wimbo wa *Nenda Salama* wa Omari Kopa

Wimbo *Nenda Salama* unaimbwa na mamake Bi. Harusi siku ya harusi ya mwanawe kumuaga na kumpa ushauri katika hatua mpya anayoingia ya ndoa. Ushauri huu ametolewa kwa njia mbalimbali ambazo zimechanganuliwa kwa kina katika sehemu hii. Kulingana na Pierce (1998), msimbo wa kisemantiki unahusika na namna ambayo ishara zinazobeba maana ambayo inaeleweka kwa haraka na kwa njia ya moja kwa moja. Hivyo, ujumbe wa ushauri kwa mwanandoa uliotolewa katika wimbo huu umewasilishwa kwa njia ya moja kwa moja. Katika kifungu kifuatacho, Bi. harusi anashauriwa wa moja kwa moja kuhusu yale yanayotarajiwa kwake anapoingia katika ndoa. Mwimbaji anasema;

Mama kawatunze wakwe zako

Mwanangu unaondoka ee
 Mama kampende mume wako
 Mwanangu unaondoka eeh

Kauli hizi za mwimbaji katika dondoo hili ni za ushauri wa moja kwa moja kwa Bi. harusi katika hatua yake mpya ya maisha. Msanii anamshauri Bi. harusi kumpenda mume wake kwani ndiye aliyemtoa kimasomaso kutoka kwao na kuanza maisha ya ndoa naye. Bi. Harusi anayo majukumu mengine mbali na kumpenda mumewe. Anapoenda kwa kina mume kuanza maisha ya ndoa, anawakuta kule ndugu pamoja na wazazi wa mumewe. Hana budi kuwapenda na kuwatunza wazazi wa mumewe kwani ndio waliomtunza na kumlea vyema mume huyu ambaye mwanamwali huyu amempenda na kuingia katika ndoa naye. Hii ndio maana mwimbaji anamtaka awatunze wakwe zake.

Kwa kusisitiza ushauri wa mapenzi ya mke dhidi ya wakwe zake, mwimbaji anatumia jazanda ya boga. Matumizi ya jazanda kuwasilisha ujumbe fiche wa kifasihi yanaafiki maelezo ya Barthes (1997) anayesema kuwa, msimbo wa kiseme unahusisha matumizi ya mbinu kisanaa zinazofumbata maana maalum katika jamii fulani. Hivyo, mbinu ya jazanda imetumika katika wimbo huu kufumbata maana ya ushauri wa ndoa kwa Bi. Harusi. Mwimbaji anasema;

Boga ulilolipenda mwanangu lipende na ua lake
 Bwana uliyempenda umpende na ndugu zake
 Lolote likikushinda mwanangu uende kwa wazazi wake

Msanii ana maana fiche anapotumia kauli *boga ulilolipenda mwanangu penda na ua lake* katika dondoo hili. Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2013), boga ni tunda ambalo huliwa baada ya kupikwa na ambalo mmea wake hutambaa na majani yake ni mboga. Hapa, majani ya tunda hili ndio maua yake yanayolipamba na kulipa mvuto.

Hivyo basi, yeyote anayelipenda tunda hili la boga bila shaka atayapenda majani yake na kuyala kama mboga kwani ni vitu viwili vinavyoenda sambamba. Msanii katika kifungu hiki ametumia jazanda ya boga na ua lake kuelezea watu wanaoenda sambamba yaani mke, mume pamoja na wazazi na ndugu wa mume na namna wanavyopaswa kuhusiana. Anamshauri Bi. Harusi kuwa anapompenda mume (ambaye amerejelewa kama boga) basi awapende pia ndugu na wazazi wake (ambao wamerejelewa kama ua) ambao wote wamefungamanishwa na huyu mume. Hii ndio maana ya kulipenda boga na ua lake ambayo msanii amesema katika kifungu cha wimbo huu. Aidha, msanii anaonyesha umuhimu wa kufanya hivi anaposema kuwa wakati wowote mke atapata ugumu wowote katika ndoa yake, atakuwa na uhuru na wepesi wa kuenda kwa wazazi wa mumewe na kushauriana nao kwani wana uhusiano mwema kutokana na anavyowaonyesha mapenzi.

Kwa upande mwingine, msanii anatoa ushauri wa ndoa kwa mwanamwali kwa njia ya moja kwa moja akifungamanisha na uhalisia wa maisha. Msanii anachora taswira kamili ya uhalisia wa maisha na kumwonyesha Bi. Harusi kuwa, ndoa ni sehemu ya maisha naye kama mke ana jukumu la kufanya kila juhudi ili kuifaulisha. Msanii anasema;

Haya yote ni maisha mwanangu kajitahidi
Yasije kubabaisha mwanangu kuchekwa huna budi
Mgawie visokwisha mwanangu mzidishie mudi

Katika kifungu hiki, msanii anamshauri Bi. harusi kwa njia ya moja kwa moja kuwa, anapoingia katika ndoa, atie bidii kuhakikisha kuwa imefaulu. Pindi tu anapofunga pingu hizi za ndoa, wanajamii huwa tayari kuanza kuitathmini ndoa hiyo iwapo itafeli au kufaulu. Msanii huyu anasema kuwa pindi tu ndoa inaanza kumyumbisha, lazima wanajamii watamcheka. Ushauri huu unalenga kumuonyesha kuwa kila afanyacho katika

ndoa yake kina athari kwake na jamii kwa ujumla, hivyo, ni jukumu lake kuhakikisha kuwa amefanya kinachohitajika ili kuepuka aibu ya kuchekwa. Mojawapo ya mambo ambayo msanii anamshauri bi harusi ni kuhakikisha ameboresha hisia za mumewe kila mara. Katika wimbo, msanii ametumia ishara *mudi* ambayo ameitohoa kutoka Kiingereza *mood* iliyo na maana ya hali ya hisia ya mtu kama vile ya furaha, huzuni na nyinginezo. Hivyo, ili kufanikisha mambo mengi kuwa bora katika ndoa, Bi. Harusi anashauriwa kumzidishia hali ya hisia mumewe kwa kuifanya iwe ya furaha mara nyingi.

Vilevile, msanii anamtahadharisha Bi. Harusi kuhusu wanaume watakaomtia majaribuni kwa kumtaka kimapenzi anapokuwa katika ndoa yake. Tahadhari hii anaitoa kwa njia ya kijazanda kwa kutumia ishara ya videge. Katika kifungu kifuatacho anasema;

Kuna videge viwili vitakuja na tishio
Vitajiletajileta kwa njia ya matamano
Jua raha ya mapenzi mwanangu ulale na mumeo.

Barthes (1977) akichangia nadharia ya Simiotiki anasema kuwa maana ya ishara fulani inaweza kutokana na mfumo ambao ishara hiyo imetumika. Hii inamaanisha kuwa ili kubainisha mana inayoashiriwa na ishara fulani, lazima uosome au kusikiliza muktadha mzima ambao ishara hiyo imetumika. Hivyo basi, katika kifungu kilicho hapo juu, ishara ya videge iliyotumika inaashiria wanaume. Maana hii inatokana na usomaji wa muktadha mzima ambamo ishara hii imetumika. Katika kifungu hiki, mwimbaji anasema kuwa vipo videge viwili ambavyo vitakuja na tishio na kujileta kwa nia ya matamano. Kauli ya mwisho katika kifungu hiki inayosema, *jua raha ya mapenzi mwanangu ulale na mumeo* inakamilisha maana ya awali katika kifungu na kuonyesha kuwa videge vinavyorejelewa katika muktadha huu ni wanaumue. Hii ndiyo maana mwanamwali huyu anashauriwa

kuepukana na videge (wanaume) hivi na asishiriki tendo la ndoa navyo kwani raha ya mapenzi ni kushiriki tendo hilo la ndoa na mumewe pekee yake. Aidha msanii huyu anazidi kumshauri mwari huyu kwa kutumia mbinu ya taswira. Anamchorea picha kamili ya kule Pwani anakoenda kuolewa na kumtahadharisha kuhusu uhalisia wa kule na kumtaka awe makini anapokuwa huko. Katika kifungu kifuatacho anasema;

Kweupe kule pwani kweupe kuna madege kweupe
Kweupe kule pwani kweupe kuna madoa kweupe
Kweupe kule pwani kweupe kuna njiwa kweupe

Kama ilivyoelezwa hapo awali katika sura hii kuwa, neno ‘madege’ au ‘videge’ limetumiwa na msanii katika wimbo huu kuashiria wanaume. Hivyo, katika dondoo hili, mwimbaji anajaribu kumchorea Bi. Harusi taswira ya kule pwani anakoenda anapoingia ndoani. Anamwonyesha kuwa, licha ya kuwa kule pwani ni kweupe yaani kuzuri, kuna wanaume (madege) wa kumtaka kimapenzi ambao anapaswa kuchungana nao ili kuulinda ndoa yake.

Mbali na hayo, msanii anatumia ishara ya ‘njiwa’ kufumbata mafunzo ya ndoa kwa Bi. Harusi katika kifungu hiki. Giliardi na wenzake (2018) wamefanya utafiti kuhusu ndege aitwaye njiwa. Katika utafiti wao, wamebainisha kuwa, njiwa ni aina ya ndege anayeishi kwa kundi na hutumia sauti tofauti za kitaswira zinazoonyesha mfumo wa kijamii. Pia, wameonyesha kuwa, njiwa ana hulka ya kuhusiana vyema na wenzake na huishi maisha ya kijamii. Hivyo basi, msanii wa wimbo huu ametumia ishara ya njiwa kijazanda kumshauri mwanamwali huyu kuhusu uhusiano mwema na jamaa za mumewe ambao anaotakiwa kuwa nao kule pwani anakoenda kuolewa. Anamkumbusha kuwa kule pwani aendako watu wanaishi kijamaa kama njiwa. Anawarejelea Wapwani kuwa njiwa

kuashiria namna wanavyoishi maisha yao kwa ujamaa kama njiwa. Hii ni pamoja na kushirikiana vyema na kufaana kwa njia mbalimbali. Hii ndiyo maana anampa wosia mwanamwali huyu kuwa anapoenda kule, ni sharti ajue namna atakavyotangamana na kuingiliana na Wapwani wakiwemo ndugu wa mumewe, wazazi wake, marafiki, majirani na wanajamii wote kwa ujumla.

3.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia kwa kifupi asili ya nyimbo za taarab na kelezea zaidi uchanganuzi wa maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab. Nyimbo ambazo zimechanganuliwa ni *Maji ya Uvuguvugu* wa Wachonga vinyago, *Bi Harusi* wa AT, *Ndoa* wa Aslay akimshirikisha Hadija Kopa na *Nenda Salama* wa Omari Kopa. Katika nyimbo hizi zote, maudhui ya ukungwi yaliyoangaziwa yanahusiana na namna mke anapaswa kumhudumia mumewe kama vile kumtengea maji ya kuoga ya vuguvugu, kumpenda na hata kumuandalia chakula. Aidha, suala jingine la mafunzo za ukungwi lililoangaziwa katika sura hii ni kuhusu namna mke anapaswa kuhusiana na jamaa za mumewe wakiwemo wakwe, mawifi na jamii geni ya mumewe kwa jumla. Ameshauriwa kuwapenda wakwe zake, kutangamana nao vyema pamoja na kumakinika na marafiki. Kwa ujumla, nyimbo hizi teule zinatoa wosia kwa mwanamwali wa kike kuhusu namna anavyopaswa kujipendekeza katika ndoa, pamoja na nguzo za kuifaulisha ndoa yake. Sura inayofuata imeangazia mwingiliano kati ya nyimbo teule za taarab na mafunzo ya ukungwi.

SURA YA NNE

MWINGILIANO KATI YA DHIMA YA KUNGWI KATIKA JAMII NA

MAUDHUI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilishughulikia maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Vilevile, chimbuko la nyimbo za taarab limetolewa ili kuweka bayana muktadha ambao umeongoza uchanganuzi wa data husika. Sura hii imeonyesha namna dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili inavyoingiliana na nyimbo teule za taarab. Mafunzo ya kungwi yamejikita katika kipera cha mawaidha ambapo sura hii imeonyesha namna kipera hiki cha mawaidha kinaingiliana na kipera cha nyimbo kwa kitengo cha maudhui.

4.1 Mwingiliano wa Tanzu na Vitanzu vya Fasihi

Bakhtin (1981) anasema kuwa tanzu za fasihi kwa ujumla hutegemeana na kukamilishana kwa njia moja au nyingine. Bakhtin (keshatajwa) analeza kuwa tanzu na vipera vya fasihi huingiliana kwa kuwa vimejengeka kwenye misingi ya utamaduni na urithi wa kijamii na kila kimoja kina umuhimu wa kipekee katika kuelezea na kuhamasisha maadili, imani na uzoefu wa jamii. Ingawa vipera hivi vinatofautiana kwa muundo na njia ya uwasilishaji, vyote vina uhusiano mkubwa katika misingi ya maudhui ambayo vinayaangazia. Yaliyomo yote katika vitanzu mbalimbali vya fasihi hujengeka kwenye misingi ya jamii husika hivi kwamba vipera vya fasihi vinachota malighafi kutoka katika jamii husika hivyo kuchangia katika uelewa wa jamii kwa ujumla. Bakhtin (keshatajwa) anasisitiza kuwa mwingiliano wa kimaudhui kati ya vipera vya fasihi unaleta hujumuisho wa maana

na mifumo ya kifasihi. Kulingana naye, masuala ya kijamii, kisiasa na kimaadili yanaposhirikishwa katika vipera tofautitofauti, inapanua namna ya kutafsiri maandishi mbalimbali hivyo kutoa tafsiri nyingi za kijamii.

Kwa mujibu wa Nida (2022), vipera vya fasihi vinahusiana kwa namna ya kipekee kupitia mbinu za uwasilishaji na matumizi ya mbinu za kifasihi ambazo hutumika kuwasilisha maudhui mbalimbali. Nida anazidi kueleza kuwa, vipera vya fasihi vinavyoingiliana aghalabu huchangia katika kutoa ujumbe wa kijamii au wa kiutamaduni. Ili kudhihirisha uwiano baina ya vitanzu vya fasihi, Nida (keshatajwa) anatolea mfano wa hadithi fupi na methali na kueleza kuwa hivi viwili ni sehemu ya mfumo mmoja ambapo uwiano mkubwa unapatikana katika ujumbe au maudhui yanayozungumziwa. Methali ni kipera kinachojenga hadithi inapotumika kuelezea maadili au tabia na mara nyingi hutumika kutoa mafunzo. Methali na hadithi fupi zinategemeana katika muktadha wa kimaudhui au ujumbe na hutoa nafasi kwa hadithi kuunganishwa na mifano ya kila siku ili kuhamasisha tabia njema.

Gikandi (2018) anaeleza kuwa ngano ambayo ni kipera cha hadithi, pia ina uhusiano na tanzu zingine za fasihi andishi kama vile riwaya na hadithi fupi, kwa kuwa hutumia mbinu za uandishi wa kifasihi kuzungumzia mambo ya kijamii na ya kidhahania kwa kutumia wahusika halisi au wa kiubunifu. Gikandi (keshatajwa) anasisitiza kwamba ngano na riwaya vinaweza kushirikiana kwa kuwa vyote vinajikita katika kupitisha maudhui ya kijamii kama vile, utamaduni mapambano, ushujaa na haki. Kwa upande mwingine, vitanzu vya fasihi simulizi huingiliana kwa njia moja au nyingine. Mathalan, kitanzu cha nyimbo na kitanzu cha mawaidha ni sehemu muhimu ya fasihi simulizi inayohusiana kwa

karibu ingawa kila kimoja kina sifa na mbinu zake za kipekee katika uwasilishaji wa maudhui. Nyimbo na mawaidha hutumika kuhamasisha, kufundisha na kutoa ujumbe kwa jamii lakini zinatofautiana katika mtindo na njia ya utoaji wa ujumbe. Barasa (2020) anasema kuwa, katika fasihi ya Kiswahili, nyimbo zinahusisha tamaduni, historia na maadili ya jamii na hutumika katika nyakati mbalimbali za kijamii kama vile sherehe, harusi au majanga na mara nyingi zinadhamiria kuhamasisha, kutoa burudani au kutoa mafunzo. Baraza (keshatajwa) anaeleza kwamba nyimbo ni zana muhimu za kukuza maadili ya kijamii na mara nyingi hutumika katika hali ya kijamii ili kutoa mafunzo au kutia moyo.

Khamis (2019) anafafanua mawaidha kama maneno ya busara yatolewayo na mtu mkomavu wa umri au mtu mwenye hekima na hutumika kutoa miongozo ya maisha, kuelimisha na kuboresha tabia za kijamii. Mawaidha yanaweza kutolewa kupitia methali, hekaya, nyimbo, muktadha wa majadiliano, vikao vya familia, mikusanyiko ya kijamii au katika shughuli fulani maalum za kijamii kama vile sherehe za unyago na za jando. Khamis (keshatajwa) anaeleza kuwa, mawaidha ni kitanzu cha mazungumzo kinachohusisha elimu ya kijamii na kutoa mwanga kuhusu jinsi jamii inavyoweza kutatua changamoto zinazoikumba.

Kulingana na Juslin na Sloboda (2010) nyimbo na mawaidha vinahusiana kwa karibu sana kutokana na namna vyote hutumika katika kutoa mafunzo na maadili kwa jamii. Juslin na Sloboda wanasisitiza kwamba nyimbo zinatoa mawaidha yanayoweza kuwa na nguvu ya kuathiri hali ya kiakili ya mtu vilevile kuhamasisha kuhusu mabadiliko ya kijamii kwa ujumla. Nyimbo nyingi zina maudhui yenye mawaidha kama vile kuhimiza umoja, ushirikiano

au kufanya kazi kwa bidii. Kwa mfano, nyimbo za harusi au sherehe za jamii mara nyingi huibua mawaidha ya kijamii na familia, huku zikisisitiza umoja, upendo na msaada wa pamoja. Haya yanaonyesha jinsi nyimbo na mawaidha vinavyoweza kushirikiana ili kuleta ujumbe muhimu wa kijamii.

Mbali na uwiano kati ya mawaidha na nyimbo kwa kiwango cha ujumbe au maudhui, vitanzu hivi vilevile vinawiana kwa mbinu za uwasilishaji. Nyimbo, ingawa mara nyingi hujumuisha mahadhi ya sauti na mdundo, hutumia mbinu kama vile methali, misemo, tashbihi, istitari miongoni mwa mbinu zingine kuwasilisha maudhui. Nyimbo zinajumuisha uwiano na mawaidha, ambayo pia hutumia tashbihi, istitara methali na maneno ya busara ili kutoa ujumbe muhimu. Kwa hivyo, nyimbo na mawaidha hutumia lugha ya wazi na ya moja kwa moja pia wakati mwingine lugha fiche ili kufikisha ujumbe wa kijamii au wa kimaadili.

4.2 Mwingiliano kati ya Dhima ya Kungwi katika Jamii na Maudhui katika

Nyimbo teule za Taarab.

Kama ilivyobainishwa katika sura ya tatu, dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili ni kuwafundisha wanawali kuhusu masuala ya unyumba au majukumu yao katika ndoa. Kadri muda unavyozidi kusonga, mafunzo haya yameanza kutekelezwa na baadhi ya wasanii wa nyimbo za taarab ambapo wanayaimba mafunzo haya ya makungwi katika nyimbo husika. Hili linaibusha suala la mwingiliano matini hivi kwamba mafunzo ya makungwi kama kitanzu cha mawaidha kinaingiliana na kitanzu cha nyimbo katika wanda pana la fasihi simulizi. Katika sehemu hii, kwa kuongozwa na nadharia ya Uamilifu, mwingiliano kati ya vitanzu hivi viwili umejadiliwa kwa vitengo vitatu

ambavyo ni uhusiano wa mke na mumewe, uhusiano kati ya mke na jamaa za mume na kujitunza kwa mke.

Nadharia ya uamilifu ni mtazamo wa kijamii na kiufasihi unaojikita katika kuelewa jinsi vipengele mbalimbali vya jamii au tamaduni vinavyofanya kazi ili kudumisha utulivu, mfanano na utendaji mzuri wa jamii hiyo. Nadharia hii inazingatia umuhimu wa mfumo ya kijamii na jinsi vipengele vyake vinavyoshirikiana ili kudumisha utaratibu na kujenga ufanisi wa kijamii kwa ujumla. Kwa mujibu wa Jakobson (1960), Uamilifu unaeleza namna jamii inavyofanya kazi kama mfumo unaohusiana, ambapo kila sehemu inachangia kwa namna fulani katika utendaji wa jumla. Katika muktadha wa fasihi, nadharia hii inatumika kudhihirisha kuwa vitanzu vya fasihi ni sehemu za mfumo mkubwa vinavyoshirikiana ili kufanikisha malengo ya kifasihi kama vile kuhamasisha, kuelimisha au kutoa taarifa muhimu kwa jamii. Kutokana na hayo basi kitanzu cha mawaidha na kitanzu cha nyimbo vinaunda mfumo wenye ushirikiano kwa madhumuni ya kuelimisha, kushauri, kukashifu au kuelekeza tabia fulani katika jamii. Mafunzo anayotoa kungwi kwa mwanmwali katika jamii ya Waswahili yapo chini ya kitanzu cha mawaidha na yanaingiliana au kushirikiana na maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab ili kufanikisha malengo mbalimbali ya kijamii yakiwemo kuelimisha, kuonya na kukashifu tabia hasi miongoni mwa wanawali. Kuna uwiano mkubwa baina ya mawaidha ya kungwi kwa wanawali na ujumbe unaojitokeza katika nyimbo teule za taarab. Haya yamejadiliwa kwa kina katika sehemu ifuatayo.

4.2.1 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui ya Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Uhusiano wa Mke na Mumewe

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na makungwi wa eneo la Msambweni, data iliyokusanywa ilionyesha kuwa miongoni mwa mafunzo ambayo makungwi huwapokeza wanawali ni uhusiano wa mke na mumewe. Kulingana na makungwi, mke anapaswa kuuboresha uhusiano wake na mumewe kutokana na namna anavyomhudumia akiwa naye nyumbani. Mathalaan, kutokana na mahojiano ya mtafiti na kungwi mmoja wa eneo la Msambweni, ilijitokeza kuwa mke anapaswa kumsaidia mume katika shughuli za kujiandaa kuenda kazini kwa kumtendea mambo kadha wa kadha mojawapo ikiwa kumpelekea maji bafuni. Hata hivyo, kungwi lengwa kutoka eneo la Msambweni alisisitiza kuwa, mke ahakikishe kuwa iwapo kuna kijibaridi basi ayapashe maji hayo moto yawe ya vuguvugu. Mtafiti alipomhoji kungwi mmoja alisema;

Mume anaporauka kujiandaa kuenda kazini, ni jukumu la mke kuhakikisha kuwa amempelekea maji bafuni ambayo ni ya vuguvugu iwapo kuna baridi kisha kumpa kitambaa cha kufuta maji mwilini baada ya kuoga.

Mafunzo haya vilevile yamekaririwa na Wachonga Vinyago katika wimbo wao wa *Maji ya Uvuguvugu* ambapo wanasema kuwa mke amtengee mumewe maji ya vuguvugu ya kuoga. Kifungu cha dondoo kifuatacho kinaonyesha uwiano baina ya mafunzo wanayotoa makungwi na yale yanayoimbwa na waimbaji teule wa nyimbo za taarab.

Maji ya uvuguvugu, mtengee aoge
Mume hataki vurugu, anataka utulivu
Mpake poda mumeo, usijempaka jivu

Mstari wa kwanza wa kifungu hiki unaibua maudhui ya ukungwi yanaoeleza majukumu ya mke katika ndoa. Mke anashauriwa kumtengea maji ya uvuguvugu wala sio yale baridi

au ya moto sana na kumpelekea bafuni. Haya yanadhihirisha namna mafunzo ya makungwi yanatekelezwa na baadhi ya waimbaji wa nyimbo za taarab. Mafunzo haya ya makungwi kuimbwa na wasanii hawa inaonyesha namna nyimbo na mawaidha ni vitengo vya jamii vinavyotegemeana na kukamilishana.

Mbali na hayo, mwanamke ana majukumu makubwa kwa mumewe pindi tu anaporejea nyumbani kutoka kazini. Mke anatarajiwa kumpokea mumewe kwa mahaba anaporejea nyumbani. Haya ni kwa mujibu wa makungwi lengwa wa Msambweni waliohojiwa na mtafiti. Makungwi hawa walieleza kuwa;

“Mume anaporejea kutoka kazini, mke anapaswa kumkaribisha nyumbani kwa mahaba kwani atakuwa amechoka na huenda kukereka kazini. Anapoingia kwa nyumba, amlaki kwa kumkumbatia na kumwambia maneno matamu ya kimahaba kama vile, “Karibu ndani mume wangu, mimi hapa mkeo wa ndoa, ua lako na pambo lako la kuyafurahisha macho yako. Nikuhudumie vipi? Sijui utakula kwanza ama utakoga kwanza maana chakula ki tayari na maji ya kukoga ya vuguvugu nimeshayapeleka bafuni.”

Katika dondoo hili, mke anatarajiwa kumlaki mumewe kama ishara ya mapenzi yake kwake ili kuuhisha uhusiano wao. Vitendo vya mahaba ambavyo kungwi anamfundisha ni pamoja na kumpa chakula, kumwandalia maji ya kuoga na kumwambia maneno matamu ya kimahaba. Mafunzo haya ya unyumba kwa mke yamekaririwa na Wachonga vinyago katika wimbo wao wa *Maji ya Uvuguvugu* wanapoimba;

Akirudi kazini, mpokee
 Busu liwe shavuni, mpokee
 Mkaribishe chumbani, mpokee
 Tabasamu la usoni, mpokee
 Umbebe mgongoni, mpokee
 Kaoge naye bafuni
 Umpe yale mahaba, ulofunzwa unyagoni

Waimbaji katika kifungu hiki wanawafunza wanawari yale yanayofunzwa na makungwi na hata mengi zaidi. Mbali na mke kumpokea mume, kumpa chakula na kumwandalia maji ya kuoga, waimbaji hawa wanamshauri mke kumzidishia mume mahaba. Wanamshauri kuenda hatua moja zaidi na kumpelekea tu mume maji bafuni na kumtaka ambebe mgongoni kumpeleka bafuni na hata kuoga naye. Pia, wanamshauri mke kumpa mumewe mahaba yote aliyofunzwa unyagoni. Haya yanadhihirisha kuwa mafunzo ya unyagoni yamefungamanishwa katika baadhi ya nyimbo za taarab kama wimbo huu.

Zaidi ya hayo, mwanmwali anakumbushwa na kungwi wake kuwa, mume pia ni sawa na mtoto. Katika kulinganisha mwanamume na mtoto, wanamaanisha kuwa, kama tu mke anavyomshughulikia mtoto akiwa kwenye ndoa, ndivyo anavyostahili kumshughulikia mume. Mtoto anapaswa kuangaliwa mara kwa mara kuhakikisha kuwa ameshiba, kuangalia pia iwapo amejiendea haja na kumsafisha. Anapolia pia, huangaliwa kubaini sababu ya kilio chake. Vivyo hivyo, kungwi katika mafunzo yake anamkumbusha mwanmwali kuwa ana jukumu kubwa la kumwangalia mumewe. Kutokana na mahojiano yaliyofanywa na mtafiti na makungwi lengwa wa Msambweni, walidhihirisha haya kupitia usemi ufuatao;

Wanawake wengi wanapopata watoto katika ndoa huwasahau waume zao kabisa na kujishughulisha tu na watoto wao. Wakumbuke pia mume ni kama mtoto na anastahili kuangaliwa au kuhudumiwa pia. Zaidi ya kumshughulikia mtoto au watoto, mke anapaswa kutenga muda wake na mumewe. Kwa mfano, watoto wanapokula na kuenda kulala, huu ndio muda anapaswa kumburudisha mumewe kwa kucheza naye, kukimbizana chumbani, kumkanda na hata kutaniana naye.

Kutokana na dondoo hili, inabainika kuwa mke ana jukumu la kumtunza mumewe kama tu anavyotunza mwanawe mchanga. Katika dondoo hili, maelezo ya kungwi yamewasilishwa kwa mbinu ya tashbihi ambapo mume amelinganishwa na mtoto. Tashbihi inatumika kwa ufanisi katika fasihi ili kutoa maana zaidi na kuonyesha uhusiano kati ya vitu au hali fulani kwa njia ya picha au mifano (P'Bitek, 1973). Hivyo, mume kulinganishwa na mtoto kuna maana kuwa anapaswa kushughulikiwa kwa njia nyingi yakiwemo kuandaliwa chakula, kuangaliwa iwapo ana hitaji lolote na kuhudumiwa ipasavyo. Mafunzo haya ya makungwi yanawiana na ujumbe katika wimbo wa Wachonga Vinyago wa *Maji ya Uvuguvugu* wanaposema kuwa;

Mwanaume kama mtoto
Anahitaji kubembeleza
Aaa! Mwanaume kama mtoto
Anahitaji kubembeleza

Kifungu hiki cha mwisho katika wimbo huu kinadhihirisha namna ambavyo mwanamume alivyo sawia na mtoto mchanga anayechungwa kwa makini na mamake. Waimbaji hawa katika kifungu hiki vilevile wanaonyesha namna ambavyo mume anapaswa pia kubembeleza kama tu vile anavyobembeleza mtoto. Mume anabembeleza hasa wakati amekerwa na jambo fulani au wakati mke anapomkwaza. Ujumbe huu wa ukungwi katika wimbo huu ni ithibati tosha ya mwingiliano wa kitanzu cha nyimbo na mawaidha.

Pia, kungwi wanamfundisha mwanamwali kuhusu namna ya kusemezana na mumewe kwa madhumuni ya kudumisha uhusiano baina yao. Mawasiliano mema ndio nguzo ya ufanisi wa uhusiano mwema baina ya mume na mke. Kupitia uchunzaji, mtafiti aliweza

kushiriki darasa la kungwi na mwanamwali wake katika eneo la Msambweni na kupata mafunzo yafuatayo kuhusu namna mke anapaswa kuzungumza na mumewe;

Mwanangu, mazungumzo yako na mumeo ni muhimu sana na unapaswa kuyamakinikia kwa ustawi wa ndoa yako. Wakati kumezuka tofauti baina yako na mumeo, linda ulimi wako. Ujue ni wakati gani na mahali wapi mwafaka pa kusuluhishia tofauti zenu. Kumbuka kuwa kitanda cha ndoa sio jukwaa la kutatulia tofauti zenu bali ni uga wa mahaba. Katika kuzungumza na mumeo, zingatia sana toni ya mazungumzo yako kwake. Kumbuka kuwa huyo mume wako sio mwanasiasa wa bungeni au mshindani wako wa *debate* za shuleni hivyo, epuka sana hoja za mabishano yasiyo na msingi.

Katika dondoo hili, mawaidha yanayotolewa na kungwi yanamtaka mke kuwa makini kila anaposhiriki mazungumzo na mumewe ili kuepusha mvutano au migogoro ya namna yoyote ile. Anashauriwa kuwa na uwezo wa kubaini wakati na mahali mwafaka pa kutatua tofauti yoyote inayojiri baina yake na mume. Anamuonya kuhusu kutatulia tofauti zake na mumewe kwenye chumba chao cha kulala. Halikadhalika, kungwi anamuonya mwanamwali wake kuhusu kushiriki mashindano na mumewe kana kwamba ni mwanasiasa mwenzake au mshindani wake katika mijadala ya shule. Haya vilevile yanakaririwa na Aslay pamoja na Hadija Kopa katika wimbo wao wa *Ndoa*. Kifungu kifuatacho kinadhihirisha haya;

Usipende kugombana na mume wako
Hata kama kuna kitu kimekukwaza
Rudi vikizidi vituko, ama nyumbani kwako hujafukuzwa

Mstari wa kwanza hapa unatoa onyo kwa mke kwamba aepuke ugomvi na mumewe kwa vyovyote vile. Asiangelie uzito wa lolote lile linalotokea baina yake na mumewe likamfanya kumkosea mumewe heshima kwa kumkoromea au kugombana naye. Anamshauri kuwa iwapo yatamshinda zaidi ni afadhali arudi nyumbani kwao. Kifungu

hiki cha wimbo kuhusu namna ya mke kusema na mumewe kinaonyesha uwiano wa kipera cha mawaidha na nyimbo kuhusu dhima yao.

4.2.2 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui katika Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Uhusiano kati ya Mke na Jamaa za Mumewe

Mbali na kumfunza mwanamwali kuhusu namna ya kuhusiana na mumewe, makungwi wanalo jukumu jingine la kuwafundisha mwanamwali kuhusu uhusiano wake na jamaa za mumewe wakiwemo mawifi, mashemeji, baba na mama mkwewe, marafiki na hata jamii yake kwa ujumla. Kwa kuwa mtu ni watu, mke anapolewa na mume na bila shaka anatangamana na jamaa za mume kule. Hii ndio maana kungwi humfunza pia jinsi ya kuhusiana na watu wanaomzunguka mume. Mafunzo haya yalitolewa ifuatavyo na makungwi lengwa ambao mtafiti aliwahoji;

“Ni marufuku kuzitoa siri zako na mumeo kwa watu mwanangu. Usifikiri kuwa kila unayemwambia kuhusu ndoa yako anaifurahia, utaiharibu ndoa yako mwenyewe kwa ulimi wako. Pima kabisa kila unachosema na marafiki zako. Usiseme udhaifu wa mumeo kwa watu. Watunze, wapende na kuwaheshimu sana wazazi na ndugu wa mumeo. Mwanangu, unakwenda kuolewa, kule unakoenda kuishi kumbuka sio kituo cha redio wala televisheni ukaanze kusambaza habari za ndani kwa umma. Umbeya ni uchafu na sumu kali katika ndoa. Linda kinywa chako unapokuwa na watu wengine maana hao unaodhani ni marafiki watakushauri umuache mumeo ili wamchukue. Iga mfano wa mtungi na kata yake mwanangu.”

Katika nukuu hii, inabainika kuwa ni wajibu wa mke kuchuja kile anachokisema kwa marafiki kumhusu mumewe pamoja na ya chumbani mwao. Anakumbushwa kuwa, ulimi wake ni kiungo kidogo sana kwenye mwili wake ila kinaweza kuichoma nyumba yake. Yale anayosema kwa marafiki yanaweza kumchongea na kuiharibu ndoa yake. Hivyo, mke anashauriwa kuwa makini na jinsi anavyotangamana na marafiki zake na yale

anayosema nao. Mafunzo haya ya uhusiano baina ya mke na jamaa za mume pia yamejitokeza katika wimbo wa *Ndoa* wao Aslay na Hadija Kopa. Waimbaji hawa wanasema;

Mashoga, wataiharibu ndoa yako
Watakupindua, watamteka mume wako
Jitahidi uwaheshimu wakwe zako
Hizo ndizo nguzo za kutunza ndoa yako

Kulingana na Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2013), shoga ni rafiki wa kike wa mwanamke hivyo mstari wa kwanza unaosema *mashoga wataiharibu ndoa yako* unawarejelea marafiki wa kike wa mke ambao anapaswa kuwa makini nao. Anatahadharishwa kuhusu kuwaamini sana marafiki zake kwa kiasi cha kuwafichulia siri za ndoa yake na za kumhusu mume. Anakumbushwa kuwa, anapowafichulia marafiki siri za mumewe ndipo anapofungua mwanya wa wao kumfahamu na kubainisha mbinu za kumteka.

Katika dondoo hili pia, inabainika mafunzo zaidi kuhusu namna mke anavyostahili kuhusiana na jamaa wa karibu wa mume ambao ni wazazi na ndugu zake. Kauli ya kungwi isemayo *jitahidi uwaheshimu wakwe zako* ni nguzo muhimu kwa mke anapoingia katika ndoa anamkumbusha kuwa, anapoingia katika ndoa na mumewe, atawakuta wazazi pamoja na ndugu za mume. Anatakiwa basi kuwaheshimu wote ili kuishi nao vyema na kuepusha migogoro ya aina yoyote kati yake nao. Mafunzo haya ya heshima na uhusiano mwema kati ya mke, ndugu na wazazi wa mume vilevile yamekaririwa na Omari Kopa katika wimbo wake wa *Nenda Salama* katika vifungu viwili vifuatavyo anaposema;

Mama kawatunze wakwe zako
 Mwanangu unaondoka ee
 Mama kampende mume wako
 Mwanangu unaondoka eeh

Boga ulilolipenda mwanangu lipende na ua lake
 Bwana uliyempenda mwanangu umpende na ndugu zake
 Lolote likikushinda mwanangu uende kwa wazazi wake

Mstari wa kwanza katika kifungu cha kwanza unatoa mafunzo kwa mwanmwali kuwa anapoingia katika ndoa analo jukumu la kuwatunza wakwe zake. Mama na baba mkwewe ndio wazazi wake wapya anapokuwa kwa mumewe hivyo mke anafahamishwa kuwa anapaswa kuwatunza kwa njia nyingi kama vile kuwasaidia majukumu ya nyumbani panapobidi. Aidha, kifungu cha pili kinatoa mafunzo kwa mke kuwapenda ndugu na wazazi wa mume kwa ujumla. Hii imedhihirika kupitia kauli ya mwimbaji huyu kuwa *Boga ulilolipenda mwanangu lipende na ua lake, bwana uliyempenda umpende na ndugu zake*. Haya yanadhihirisha kuwa mwanamwali anapompenda mwanaume na hatimaye kufunga ndoa naye, hana budi kuwapenda ndugu na wazazi wake ili kuistawisha ndoa yao. Nukuu za makungwi lengwa waliohojiwa na za waimbaji wa nyimbo teule za taarab zinadhihirisha kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya haya mawaidha ya kungwi na maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Hii ni ishara tosha ya kuwepo kwa mwingilianomatini baina ya vipera vya mawaidha na nyimbo.

4.2.3 Mwingiliano wa Dhima ya Kungwi na Maudhui katika Nyimbo Teule za Taarab kuhusu Kujitunza kwa Mke.

Dhima nyingine muhimu ya kungwi ni kumfunza mwanmwali kuhusu usafi wake binafsi. Kutokana na mahojiano ya mtafiti na makungwi lengwa, ilijitokeza kuwa mke ana

jukumu la kuhakikisha kuwa ni msafi na mwenye mvuto kila mara. Anapaswa kujitahidi kupendeza machoni mwa mumewe. Kungwi mmoja alieleza haya;

Mke anapaswa kuzingatia usafi wa mwili ili kumvutia mumewe kila mara. Mara nyingi wanawake wengi baada ya kujifungua hata mtoto mmoja, hujisahau na kuacha kujinadhifisha kabisa. Baada ya kumshughulikia mtoto kama kumlisha au kumlea, aoge mara kwa mara na kubadilisha mavazi yake ili awe na mvuto kwa mumewe. Anapaswa kuonekana mpya kila siku machoni mwa mumewe.

Ujumbe katika dondoo hili unamsawiri mwanamke kama pambo la mume. Katika shughuli zake za malezi zikiwemo kumnyonyesha mtoto, kumlisha na hata kumlea hupata kuchafuka mara kwa mara kwa mkojo, matapishi au hata kuchafuliwa na chakula. Hivyo basi mke anakumbushwa kuwa ni jukumu lake kuhakikisha kuwa ameoga mara kwa mara kujirashia kwa manukato na kubadilisha nguo zilizochafuliwa wakati wa kumshughulikia mtoto. Haya yatampa mumewe mvuto mara kwa mara hivyo kudumisha upendo baina yao. Aslay na Hadija Kopa vilevile wanayafunza haya katika wimbo wao wa Ndoa wanaposema;

Wa kusihi usiendekeze takutoa roho
Lakini usiwe kama zeze kwenye ndoa yako
We jitahidi upendeze uwarushe sana roho
Ila bali usicheze na mume wako

Kifungu hiki kinaibua ujumbe kwa mke kuzingatia usafi wake sana ili apendeze. Msatari wa tatu wa kifungu hiki unasema *we jitahidi upendeze uwarushe sana roho*. Unadhihirisha kuwa mke hana budi kupendeza kila mara kwa vyovyote vile. Usafi wa mke ni sifa inayosisitizwa na makungwi katika mafunzo yao vilevile waimbaji hawa katika wimbo wa ndoa. Hili linaonyesha namna vipera hivi viwili; mawaidha na nyimbo vinavyoingiliana kimaudhui.

4.3 Hitimisho

Sura hii imeangazia namna mafunzo ya kungwi au mawaidha katika jamii yanaingiliana na maudhui ya nyimbo teule za taarab. Imeanza kwa kubainisha muktadha wa kulijadili lengo hili kwa kuangalia namna tanzu na vitanzu vya fasihi vinavyoingiliana kwa ujumla. Sehemu iliyofuata imeonyesha namna mafunzo ya kungwi ambayo ni kitanzu cha mawaidha kinavyoingiliana na maudhui katika nyimbo teule za taarab. Mwingiliano huu umebainika kwa kiwango cha namna mke anavyostahili kuhusiana na mume, namna mke anavyostahili kuhusiana na jamaa za mume na uzingativu wa usafi wa mke. Katika vitengo hivi vyote, imebainika kuwa nyimbo teule za taarab zilizochanganuliwa, zinahusiana kwa karibu sana kimaudhui na mawaidha ambayo makungwi huwapa wanawali. Sura inayofuata itashughulikia hitimisho la tasnifu hii ambapo muhtasari, changamoto za utafiti na mapendekezo ya utafiti wa baadaye vimetolewa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Sura hii inahusu muhtasari wa matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti wa baadaye. Kwa ujumla, imegawika katika sehemu tano ambazo ni muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, changamoto za utafiti na mapendekezo kuhusu utafiti unaoweza kufanywa baadaye.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulinuia kuchunguza maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab. Mtafiti alikuwa na malengo matatu ambayo alidhamiria kuyatimiza. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili, la pili likawa kuchunguza maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab nalo la tatu likahusu kutathmini mwingiliano kati ya dhima ya kungwi katika jamii na maudhui katika nyimbo teule za taarab.

Utafiti huu umewasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza imeshughulikia sehemu kuu ambazo ziliupa msingi utafiti wetu. Sehemu hizi ni pamoja na usuli wa mada ambao umeweka bayana dhana ya nyimbo za taarab, dhana ya kungwi na utamaduni wa mafunzo ya makungwi katika jamii ya Waswahili hivyo kuweka wazi muktadha mwafaka wa utekelezaji wa malengo ya utafiti. Pia, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti vimeshughulikiwa. Sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka pamoja na tahakiki

kuhusu mada viliangaziwa kwa ukamilifu. Nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu zimejadiliwa ambazo ni Simiotiki na nadharia ya Uamilifu. Halikadhalika, mbinu za utafiti zimeshughulikiwa katika vitengo vya eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo. Sura ya kwanza imekamilika kwa kubainisha maadili ya utafiti ambayo yamemuongoza mtafiti katika mchakato mzima wa utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili ambapo historia fupi ya jamii ya Waswahili imetolewa ili kuibua uelewa wa muktadha wa utafiti na utekelezaji wa lengo husika. Sehemu nyingine iliyoangaziwa katika sura hii ni mafunzo mbalimbali ya kungwi kwa mwanamwali ambapo yamejadiliwa kwa kina katika vitengo kadha wa kadha. Kitengo cha kwanza ni namna ya mke kumhudumia mume ambapo majukumu mbalimbali ya mke yameelezwa kwa kina. Kitengo cha pili kimeshughulikia mafunzo ya vifaa mbalimbali na maana yake ambapo vifaa vilivyoangaziwa ni mbuzi, ufagio, kanga, shanga, vikuku na kinu. Vitengo vingine vimehusisha namna ya mke kuhusiana na watu wengine, namna ya kuzungumza na mume, usafi wa kuzingatiwa na mke kisha maelezo kuhusu adhabu wanayopokezwa wanawali wasiotii mafunzo ya makungwi.

Sura ya tatu imeshughulikia maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab. Sura hii imetangulizwa kwa kuweka bayana asili ya nyimbo za taarab ili kuonyesha namna zinavyofungamana na utamaduni wa Waswahili. Kitengo kilichofuata katika sura hii ni uchunguzi wa maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Haya yamepangwa kwa utaratibu ambapo maudhui ya ukungwi yamechunguzwa katika wimbo

wa *Maji ya Uvuguvugu* wa Wachonga Vinyago, wimbo wa *Bi. Harusi* wake AT, wimbo wa *Ndoa* wake Aslay na Hadija Kopa kisha wimbo wa *Nenda Salama* wake Omari Kopa.

Sura ya nne imetathmini mwingiliano wa dhima ya kungwi katika jamii na maudhui katika nyimbo teule za taarab. Sehemu ya kwanza ya sura hii imeonyesha namna tanzu na vitanzu vya fasihi vinaingiliana. Sehemu iliyofuata imeonyesha tathmini ya namna kitanzu cha mawaidha ambayo ni mafunzo ya kungwi kinavyoingiliana na kitanzu cha nyimbo. Haya yamejadiliwa katika vitengo vikuu vitatu ambavyo ni mwingiliano wa dhima ya kungwi na maudhui katika nyimbo teule za taarab kuhusu uhusiano wa mke na mumewe, uhusiano wa mke na jamaa za mumewe na kujitunza kwa mke.

Hatimaye sura ya tano imejikita katika kutoa hitimisho la utafiti mzima. Hitimisho hili limetoa muhtasari wa sura zote zilizomo katika utafiti mzima. Vilevile, limejumuisha matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo, changamoto zilizokumba utafiti kwa ujumla na mchango wa utafiti katika ulingo wa usomi. Sura hii imekamilika kwa kutoa mapendekezo mbalimbali kuhusu tafiti ambazo zinaweza kufanywa na watafiti wengine katika siku zijazo.

5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo

Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha dhima ya kungwi katika jamii ya Waswahili. Hapa utafiti ulibainisha kuwa, dhima kuu ya kungwi katika jamii ya Waswahili ni kumfundisha mwanmwali kuhusu masuala ya unyumba yanayohusu ndoa. Kutokana na mahojiano na uchunzaji ambao ulitekelezwa na mtafiti katika eneo la Msambweni kaunti ya Kwale, maelezo mbalimbali kuhusu mafunzo ya unyumba yalitolewa na makungwi lengwa wa

utafiti. Makungwi hawa walieleza kuwa, mke ana jukumu la kumhudumia mumewe kwa njia anuwai. Njia hizi zilizojadiliwa ni kumsaidia wakati anapojiandaa kuondoka kwa nyumba kwenda kusaka riziki kwa kumpelekea maji ya vuguvugu bafuni, kumpangusia viatu vya kuvaa na kumwandalia nguo ya kuvaa. Njia nyingine ya kumhudumia mume iliyojadiliwa ni mke kumlaki mume anaporejea kutoka kusaka riziki, kumpelekea maji ya kuoga bafuni, kumwandalia chakula na kutenga muda wa kushiriki mahaba naye.

Aidha, ilibainika kuwa, dhima nyingine ya kungwi ni kutoa mafunzo kwa mwanamwali kuhusu namna ya kutumia vifaaa mbalimbali vya kitamaduni kama vile kinu, mbuzi, shanga, kanga, vikuku na ufagio. Utafiti umeonyesha kuwa vifaa hivi vyote ni jazanda kwani vina maana yake dhanishi (ya kimsingi) na ile ya ziada ambayo ni fiche kwani inahusu masuala ya ndoa. Pia, imedhihirika kuwa mke anapaswa kuvitumia kwa njia ipasavyo anapokuwa katika nyumba yake ili kuhuisha mapenzi yake na mumewe.

Aidha, utafiti ulibainisha kuwa dhima nyingine ya kungwi ni kumfundisha mwanamwali kuhusu namna ya kuhusiana na watu wengine. Mafunzo haya yaliweka wazi kuwa wakati mke anapoenda kuolewa kwa kina mume, anawakuta jamaa za mume kule kama wazazi wa mume, ndugu zake pamoja na marafiki. Kulingana na maelezo ya makungwi lengwa, mke huyu analo jukumu la kuwapenda, kuwatunza na kushirikiana nao vyema ili kustawisha ndoa yake. Pia, mazungumzo ya mke na mumewe yamefafanuliwa ambapo mke anashauriwa kufahamu wakati na mahali pa kutatulia migogoro yake na mumewe.

Masuala yaliyojadiliwa katika sehemu ya mwisho ni kuhusu usafi na adhabu kwa wanawali wasiotii. Kuhusiana na usafi mafunzo ya kungwi yameonyesha kuwa mke

anapaswa kuzingatia usafi wa mwili wake vilevile nyumba yake kila wakati. Haya ni kwa ajili ya kumvutia mumewe kwake na hata na hivyo kusaidia kuepusha mchepuko katika ndoa kwani mume hawezi kuwa na sababu yoyote ya kuvutiwa na vya nje. Mbali na kutoa mafunzo haya yote kwa wanawali, imebainika pia makungwi wanalo jukumu jingine kubwa la kuwaadhibu wanawali wasiotii. Mwanamwali asiyetii mafunzo ya makungwi wake amerejelewe kama *mwalibewa*. Hawa ndio wanaopokezwa kichapo na kungwi wao kila anapopewa ripoti za kutotii kwao na ili kuwarekebisha anawarudisha unyagoni katika mafunzo tena.

Lengo la pili lilihusu uchunguzi wa maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab. Katika wimbo wa *Maji ya Uvuguvugu* wa Wachonga Vinyago, maudhui ya ukungwi yamebainika kwa njia ya moja kwa moja kwa kuonyesha kuwa mke ana majukumu mbalimbali katika ndoa yake. Haya ni pamoja na kumwandalia mumewe maji ya uvuguvugu kila anapohitaji kuoga, amtunze vizuri kuepusha kunyakuliwa na “kunguru” (wanawake wengine), kuyabana ya chumbani mwake na mumewe wala sio kuzagaza kwa marafiki zake pamoja na kumpokea vyema anapotoka kazini.

Katika wimbo wa *Bi. Harusi* wake AT, maudhui ya ukungwi yamejitokeza kwa njia ya kejeli na ya kijazanda. Kwa njia ya kejeli, mke amepokezwa mafunzo ya namna ya kuhusiana na jamaa za mume kwa kuzoea utani na sio kukasirika ataniwapo. Pia, kupitia kukejeliwa kwa kupika wali mbichi na nyama chungu, anafunzwa jukumu lake kuu la kujua mapishi. Aidha, kijazanda mke anafundishwa namna ya kuhusiana na wakweze wala sio kuwasema vibaya.

Katika wimbo wa *Ndoa* wao Aslay na Hadija Kopa, mafunzo ya ukungwi yamedhihirika ambapo mke anaonywa dhidi ya kuitia ndoa doa kwa njia yoyote ile ili kuepusha aibu. Pia, anamfunza mke kuwa msiri katika ndoa na kuwa mwangalifu sana na marafiki zake kwani wanaweza kupokonya mumewe iwapo atakuwa akiwapa siri zote za mumewe. Wimbo huu umemuonya mke pia kuhusu kuyaanika masuala ya ndoa yake kwenye mitandao ya kijamii kama vile *Whatsapp* kwani yaweza kuwa jukwaa la kumpotezea mume.

Hatimaye, wimbo wa *Nenda Salama* wa Omari Kopa vilevile umeibua maudhui ya ukungwi kwa njia anuwai. Mke anakumbushwa kuwapenda na kuwatunza wakwe zake anapoigia katika ndoa. Pia, anafahamishwa kuwa anapompenda mume basi ampende pamoja na ndugu na jamaa zake. Haya yameelezwa kwa kutumia jazanda ya kulipenda boga na ua lake. Aidha, mafunzo mengine ya ukungwi yanatolewa kwa kumhimiza mke kuhusu kumakinika kuhusu wengine wa kumviziavizia mumewe kwa kusudi la kumnyakua. Mafunzo haya yametolewa kwa kutumia jazanda ya *madege* ambao ndio hawa vimada wa kumnyakua mume wa wenyewe.

Kwa upande mwingine, lengo la tatu lilihusu namna dhima ya kungwi katika jamii inaingiliana na maudhui katika nyimbo teule za taarab. Utafiti umeonyesha kuwa, mafunzo anayotoa kungwi kwa mwanamwali yanagawika katika kitanzu cha mawaidha chini ya utanzu mkuu wa mazungumzo katika fasihi wanda la simulizi. Nyimbo nazo kwa upande mwingine ni kitanzu chini ya utanzu mkuu wa ushairi simulizi katika fasihi simulizi. Kutokana na haya, imedhihirishwa katika utafiti huu kuwa kuna uwezekano wa vitanzu mbalimbali vya fasihi simulizi kuingiliana au kuwiana kama vilivyo vitanzu hivi

vya mawaidha na nyimbo. Lengo hili lilitimizwa kwa kuonyesha kuwa mafunzo ya ukungwi yanayotolewa na makungwi katika jamii ya Waswahili, yanajitokeza pia katika baadhi ya nyimbo za taarab. Nyimbo hizi teule zilizodhihirisha haya ni wimbo wa *Maji ya Uvuguvugu* wa Wachonga Vinyago, *Bi. Harusi* wa AT, *Ndoa* wa Aslay na Hadija Kopa na *Nenda Salama* wa Omari kopa.

Kwa ujumla, utafiti huu umeonyesha kuwa yapo masuala yalioelezwa na makungwi waliohojiwa katika utafiti ambayo pia yameimbwa katika nyimbo teule za taarab. Masuala haya ni pamoja na mke kumhudumia mumewe kwa kumtengea maji ya kuoga bafuni, kumwandalia chakula, kumlaki arejeapo kutoka kazini na kumtengea muda wa mahaba. Suala jingine ambalo limejitokeza katika vitanzu hivi vyote ni la kutoizagaza siri ya ndoa kwa watu, kumakinika na marafiki wanaoweza kunyakua mume wa mtu, kudhibiti matumizi ya mitandao ya kijamii na kuhusiana vyema na jamaa za mume. Hata hivyo, suala la matumizi ya vifaa vya kitamaduni kama mbuzi, ufagio, vikuku na vinginevyo halijaangaziwa na waimbaji wa nyimbo hizi teule bali makungwi peke yao.

5.3 Mchango wa Utafiti

Wakongwe wa jamii ambao ndio ghala kuu la kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kama mawaidha wanapofariki dunia basi kazi hizo pia hufa pamoja nao. Kwa kuenda nyanjani na kuwahoji baadhi ya makungwi katika jamii ya Waswahili kwenye ukanda wa Pwani ya Kenya kisha kuiandikia tasnifu hii, mtafiti ameunda kongoo muhimu ambayo haijapata kuandikiwa kwa kina. Hivyo basi, utafiti huu ni nyenzo bora ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Waswahili unaohusu masuala ya unyago.

Aidha, kutokana na utandawazi na uhamiaji wa watu mjini kwa ajili ya masomo au kusaka riziki, wapo wanawali wengi ambao wameanza kukosa mafunzo haya kutoka kwa makungwi kule kijijini. Licha ya watu kuhamia mijini, wengi wa watu huamini kuwa ni mwiko kuasi utamaduni wao. Hivyo basi, utafiti huu utalifaa kundi hili la watu wanaokosa mafunzo ya unyago kwa kungwi kijijini kwa kuwaonyesha kuwa mafunzo haya yanaweza kupatikana kwa baadhi ya nyimbo za taarab. Anayeyakosa kwa kungwi basi anaweza kuzisikiliza nyimbo hizi na kuelimika kwa kina kuhusiana na masuala ya ndoa.

Zaidi ya hayo, utafiti huu unatarajiwa kuwawekea msingi watafiti wa baadaye kwa kuzamia katika hiki kipengele cha mwingilianotanzu ambapo tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinaonyesha uwiano na mwingiliano. Hivyo, utafiti huu umechangia eneo la kiusomi la mwingiliano matini kwa kuonyesha jinsi kipera cha nyimbo huingiliana kidhima na kipera cha mawaidha.

5.4 Changamoto za Utafiti

Mtafiti alikumbana na changamoto mbalimbali katika mchakato mzima wa utafiti. Zipo changamoto zilizomkabili mtafiti nyanjani na zile za maktaba. Nyanjani, mtafiti alikabiliwa na tatizo la usiri ambapo wahojiwa wengi ambao ni makungwi walikuwa wagumu sana kusema baadhi ya mafunzo ya ndani mno hasa yanayohusu tendo la ndoa kwa sababu hayo huwa siri ya kungwi na mwanamwali wake. Haya yalimlazimu mtafiti kutoyaangazia hayo katika utafiti huu. Hata hivyo, hili halikuathiri utafiti kwa vyovyote vile kwani malengo yalitimizwa vikamilifu. Maktabani, kuliibuka tatizo la uhaba wa vitabu na majarida ya marejeleo mwafaka ya Kiswahili. Hili lilimlazimu mtafiti

kutegemea kusoma yaliyohitajika kutoka lugha ya Kiingereza na kuyatafsiri. Miongoni mwa sehemu zilizohitaji tafsiri ni nadharia. Kama inavyofahamika tafsiri hukumbwa na tatizo la kupotea kwa sehemu fulani ya maana ya awali basi hili likawa tatizo kwa mtafiti.

Aidha, ugeni wa kulitalii suala la maudhui ya ukungwi katika nyimbo teule za taarab ulimletea mtafiti changamoto za kupata marejeleo maridhawa. Hata hivyo, mtafiti alipata maarifa kutoka kwa tafiti zingine zinazohusina na utafiti huu hivyo kufaulu kutimiza malengo ya utafiti.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umejikita kwenye tathmini ya mwingiliano baina ya kitanzu cha nyimbo na kitanzu cha mawaidha yaani mafunzo ya kungwi. Umeonyesha namna vitanzu hivi viwili vinaingiliana kimaudhui na utafiti huu haujakikita kwenye kipengele cha mtindo wa uwasilishaji wa ujumbe na miundo za vitanzu hivi. Kutokana na haya, mtafiti amewapendekeza watafiti wa baadaye kutafiti kuhusu mwingiliano wa kitanzu cha mawaidha na nyimbo kwa kuangazia mtindo wa uwasilishaji wa ujumbe au pia nyimbo za aina nyingine zisizo za taarab.

Mbali na hayo, utafiti huu umeonyesha namna maudhui ya ukungwi yanavyojitokeza katika nyimbo teule za taarab na kuonyesha mwingiliano wa utanzu wa mawaidha na nyimbo kimaudhui. Kitanzu cha mawaidha chini ya utanzu mkuu wa mazungumzo na kitanzu cha nyimbo chini ya utanzu mkuu wa ushairi simulizi ndivyo vilivyochunguzwa. Hivyo basi, pendekezo kwa watafiti wa baadae ni kuwa wanaweza kuchunguza mwingiliano kati ya vitanzu au tanzu zingine za fasihi simulizi kama vile semi na hadithi.

Vilevile, utafiti huu umejikita katika fasihi simulizi pekee, pendekezo kwa watafiti wa baadaye ni kuwa wanaweza kuchunguza mwingiliano kati ya kitanzu au utanzu wa fasihi simulizi na ule wa fasihi andishi.

MAREJELEO

- Abdalla, A.R. (2018). Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo Teule za Taarab Asilia: Mifano ya nyimbo za Shakila Saidi Khamis. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Huria. Haijachapishwa.
- Alexander, J. C. (2003). *The meaning of social life: A cultural sociology*. Oxford University Press.
- Ali, R. (2022). *The Significance of Jewelry in Cultural Identity*. Journal of Cultural Studies, 18(3), 112-125.
- Ali, R.A. (2018). Matumizi ya lugha katika nyimbo za taarab: Uchunguzi wa nyimbo za Mohammed Ahmed Moh'd. Tasnifu ya uzamili Chuo kikuu cha Huria Tanzania. Haijachapishwa.
- Askew, K. M. (2002). *Perfoming the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago and London: University of Chicago Press.
- Bathes, R. (1994). *The Semiotic challenge*. University of California Press.
- Beauvoir, S. (1994). *The Second Sex*. London: Jonathan cape.
- Durkheim, E. (1893). *The Division of Labour in Society*. Paris: Alcan.
- Etzioni, A. (1993). *The Spirit of Community: The Reinvention of American Society*. Touchstone. Publisher
- Fair, L. (1996). *Identify Defference and Dance: Female Initiation in Zanzibar: 1890-1930*. In Fronters, volume 17, N. University of Nabaska Press.
- Fair, L. (2001). Pastimes and Politics Culture Communiy and Indentify in Past-Abolition Urban Zanzibar, Ohio University Press.
- Gagliardi, P.L., Rocco, C. J., & Caravaggi, A. (2018). Navigation and Homing in Pigeons: A review of evidence and theories. *Journal of Avian Biology*, 49(8), 911-924.
- Gentner, D., & Forbus, K. D. (2011). The power of Analogies in Teaching and Learning. In A. K. M. Tsai & T. H. Duffy (Eds.), *Handbook of research on educational communications and technology* (pp. 22-28). Springer.
- Giddens, A., Duneier, M., Appelbaum, R. P., & Carr, D. (2017). *Introduction to Sociology* (10th ed.). W.W. Norton & Company.
- Gikandi, P. (2018). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili: Miongozo na Ufanisi*. Nairobi: Oxford University Press.

- Gikandi, S. (2000). *Literary Theory and Criticism: The use of Satire and Parody in Kiswahili Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Gottman, J. M. (2016). *The Seven Principles for Making Marriage Work*. Harmony Books.
- Gottman, J. M., & Silver, N. (2015). *The Seven Principles for Making Marriage Work: A Practical Guide from the Country's Foremost Relationship Expert*. Crown Publishers.
- Gunter, S. (2021). *Jewelry and society: The role of Adornment in Cultural Practices*. *International Journal of Fashion and Design*, 10(4), 54-70.
- Hargreaves, D. J., & North, A. C. (2010). *Musical Development and Learning: The International Perspective*. Oxford University Press.
- Harris, T. J. (2017). *Beads in Religious Practices: Cultural Insights*. *Journal of Ethnographic Studies*, 9(3), 90-105.
- Hussein, R. (2003). *Islamic Influences on Swahili Culture*. *Journal of East African Studies*, 3(2), 110-126.
- Jakobson, R. (1960). *Linguistics and Poetics*. In T. A. Sebeok (Ed.), *Style in Language* (pp. 350–377). Cambridge, MA: MIT Press.
- Juma, A. M. (2020). *Utamaduni wa Unyago na Mabadiliko yake katika Jamii za Waswahili*. *Journal of African Studies*, 45(2), 124-137.
- Juslin, P. N., & Sloboda, J. A. (Eds.). (2010). *Handbook of music and emotion: Theory, research, applications*. City, Oxford University Press.
- Kamwendo, G. (2009). *Muziki wa Taarab: Historia na Maendeleo*. Dar es Salaam: Taasisi ya Utafiti wa Tamaduni za Kiafrika.
- Kawai, T. (2000). *Functionalism in Literature: A Study of Narrative Techniques*. Town, Tokyo University Press.
- Khamis, A. (2015). *Usiri katika Mafunzo ya Unyago: Mjadala wa Kijinsia na Utamaduni katika Jamii za Waswahili*. *Journal of Swahili Studies*, 22(1), 45-60.
- Khatib, M.S (1992). *Taarab Zanzibar, Dar es salaam*. City, Tanzania Publishing House.
- King'ei, G. K. (2010). *Msingi wa Isimujamii*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es salaam.

- King'ei, K. (1993). *Language Culture and Communication: The role of Taarab Songs in Kenya (1963-1990)*. Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Havard. Haijachapishwa.
- Kirimi, M.J. (2015). *The Transformation of Swahili Unyago and Female Genital mutilation into an Alternative Rite of Passage: A pasistructure Approach*. Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Botswana. Haijachapishwa.
- Kirkpatrick, K. (2021). *The Impact of Social Media on Communication in Relationships*. *Relationship Studies Quarterly*, 14(1), 23-35.
- Makhulo, E.O. (2015). *Mamlaka na Itikadi katika Nyimbo Teule za Taarab*. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Malinowski, B. (1922). *Argonauts of the Western Pacific*. Publisher, Routledge.
- Mbaabu, I. (1990). *The Swahili Culture: An Overview of Traditions and Customs*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mbwana, H.K. (2016). *Mabadiliko ya Nyimbo za Harusi kuenda Kaswida*. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Huria Tanzania: Dar es salaam. Haijachhapishwa.
- Mchomeki, J. (2023). *Kanga: A cultural symbol in East Africa*. *Journal of African Studies*, 15(2), 45-67.
- McNeill, D. (2005). *Gesture and Thought*. University of Chicago Press.
- Mwangangi, R. (2018). *Mafunzo ya Biashara za Mtumba na thari zake kwa Uchumi wa Taifa*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ngwabi, R. (2020). *The Role of Wisdom Figures in Community Development: A Study of Kungwi in African Societies*. *Journal of African Studies*, 45(3), 25-39.
- Nida, S. A. (2022). *The Interconnections of Oral Literature Genres in African Cultures*. *Journal of Oral Tradition*, 13(2), 45-58.
- Nyongesa, J.J (2022). *Uchunguzi wa Mafumbo katika Nyimbo za Taarab za Siti Binti Saad*. Nairobi Journal of Humanities and Sciences Volm. Nairobi. Kenya.
- Okot p'Bitek. (1973). *Artist, the Ruler*. City, Oxford University Press.
- Okpewho, (1992). *African Bloomington and Indianapo*. Indiana University press.
- Patel, A. D. (2008). *Music, Language, and the Brain*. Oxford University Press.
- Radcliffe-Brown, A. R. (1952). *Structure and Function in Primitive Society*. Free Press.

- Rajab, F.H. (2016). Chanjo ya mapenzi katika nyimbo Asilia za Seif Salim. Tasnifu ya uzamili Chuo kikuu cha Tanzania, Haijachapishwa.
- Sauda, R.M. (2022). Kuchunguza taswira katika nyimbo teule za taarab za Kimahaba za Khadija Kopa Tasnifu ya umazili. Chuo kikuu cha Huria cha Tanzania. Haijachapishwa.
- Stokes, T. (2016). *The Impact of Color in Communication: An analysis*. International Journal of Color Studies, 12(1), 22-35.
- Sumra, S. (2010). *Utamaduni wa Zanzibar na Athari zake katika Muziki wa Taarab*. City Dar es Salaam University Press.
- Tenge, S. (2019). Usimamizi wa Biashara na Athari za Mbinu za Haraka katika Utendaji wa Muda Mrefu. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Trimigham, J. S. (1960). *The influence of Islam upon Africa*. Longman Group Ltd, London.
- Wamitila, K. (2006). *Swahili Language and Culture: A global perspective*. City University Press of Africa.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO A: NYIMBO TEULE ZA TAARAB

1. Wimbo wa *Maji ya Uvuguvugu wa Wachonga Vinyago*

Mwanaume tunza, yapaswa kumtunza
 Mambo usiyabanange, ukaja kuyavurunda
 Usiwe kama msungo, mwali wewe umefunzwa
 Hata special pia yaweza kuwa mtumba

Mume usije mfuja, siri za ndani zikavuja
 Bibi mtunze mumeo kuna kunguru wa Unguja

(Kiitikio) Ooyae x4

Maji ya vuguvugu, mtengee akaoge
 Mume hataki vurugu, anataka utulivu
 Mpake poda mumeo, usije mpaka jivu
 Raha ya penzi linoge, mwanamwali usiwe na wivu
 Kamtunze mume wakooo, wala usiwe na wivu

(Kiitikio) Ooyaa ee x4

Akirudi kazini (mpokee) busu liwe shavuni (mpokee)
 Kwa udi na asumini (mpokee)
 Mkaribishe chumbani (mpokee) tabasamu la usoni (mpokee)
 Umbebe mgongoni (umpokee) kaoge naye bafuni
 Umpe yale mahaba ulofunzwa unyagoniiii

Mwanamume kama mtoto anahitaji kubembeleza x4

Ooyaa ee x4

2. Wimbo wa *Bi. Harusi* wake AT

Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi

Manyakanga mko wapi leo mje muamue kesi

Balaa ugomvi leo somo yake Bi. Harusi

Mtazameni mkwe wenu kwa bashasha na ucheshi

Balaa ugomvi leo somu yake Bi. Harusi

Umetaniwa kidogo unatoa matapishi

Balaa ugomvi leo somu yake Bi. Harusi

We jifanye mjuaji kapike wali mbichi

Balaa ugomvi leo somu yake Bi. Harusi

Nampenda Shuarina, Shuarina, Shuarina x2

Namtaka Shuarina, Shuarina, Shuarina pesa sina x2

Kina mama, mabibi na mababu nawashika masikio

Hawa wari wa sasa wanatabu waozeshwe mbiombio

Kina mama, mabibi na mababu nawashika masikio

Hawa wari wa sasa wanatabu waozeshwe mbiombio

Wanjaa ana tabia mbaya, anamsema mkwewe eti kwamba ana chawa x2

Somo ona visa vya kusikitisha, mwanamwali hana pesa anajitongozesha x2

(Kiitikio)

Somo yake mueleze na mapema, akiachika wasijepata la kusema x2

Rafiki wa siku hizi usiwaone wajuzi, wanaranda na hirizi kuyaaribu mapenzi x2

Mimi na wewe tusipeane lawama, umealikwa ya nini ukimbie na nyama x2

Eeeh mama lawama kanipa shubili kaniambia nyama x3

Dada yake Bi. Harusi yuko wapi aje hapa

Nimekuja na mzigo leo nataka kumpa

Mama yake Bi. Harusi na mumewe anacheka

Mwambie babu Hamisi asije toa talaka

Wehi mama lawama, kanipa shubili kaniambia nyama x2

Eh malova lova eh, eh malova lova eh x2

Ah we ni chai nakuharibu kwa kukutia tui tu mimi

Sambusa eti nipe, sambusa x2

3. Wimbo wa Ndoa wa Aslay na Khadija Kopa

(Ndoa ndoana ukijishebedua itakubana)

Piga tarumbeta, mwanamwali anameremeta

Sifa ninazopata, Aslay naozesha leoo

Ndoa ni jambo gumu mwanangu

Kaitunze heshima yako

Chozi linanitoka mwanangu

Eh babu harusi

Mshike taratibu sije ukafuta piko

Haraka ya nini wakati huyo ni mali yako

Yako ooh

Mwanangu uchechemee

Ulofundwa usiyaseme kwa watu (usungo huo)

Maneno umumunye

Ya chumbani usiwape faida watu mwanangu

(Kiitikio)

Ndoa usiitie doa x2

Ukiitia ndoa doa x2

Utania haya x2

Wanawake wa kisasa mnajifanya mna *Whatsapp*

Hamna muda wa kuwashughulikia waume zenu

Wacha mchezo wenzio watakuwatsap mume

Usipende kugombana na mume wako

Hatakama kuna kitu kimekukwaza (mwanamke busara)

Rudi vikizidi vituko (haja kutoa juu ya mti babaaa eeh) hapa ni nyumbani kwako
hujafukuzwa

Mashoga wataharibu ndoa yako

Watakupindua, watamteka mume wako

Jitahidi uwaheshimu wakwe zako

Hizo ndizo nguzo za kuitunza ndoa yako

Wivu uendekeze takutoa roho

Lakini usiwe kama zeze kwenye ndoa yako

We jitahidi upendeze uwarushe sana roho

Ila mbali usicheze na mume wako

(Kiitikio)

Mwanangu seketu

Seketu

Eh baba seketu

Seketu

Maulii seketu

Seketu

Nasema babu harusii ee

Mumemuona

Babu harusii ee

Mumemuona ee

Bibi harusii mumemuona x2

Baba eeh mwali ee

Mumemuona

Mmh mamae mwali ee

Mumemuona

Mwanaume harogwi

Anarogwa kwa mambo ee mambo ee

Aslay naangaika ee

Eeh nisaidie mwanangu

Naangaika

Nisaidie wanangu

Babu harusii kahangaike ee

Nisaidie wanangu

Kahangaike ee

Tusaidie wanangu

Bibi harusii kaangaike

Tusaidie wanangu

Kaangaike

Tusaidie wanangu

4. Wimbo wa *Nenda Salama* wake Omari Kopa

Nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo ushapata wako mwanangu unaondoka leoo

Nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo umepata wako mwanangu unaondoka aeheh

(Nenda mama)

Leo umepata wako mwanangu

Nasema nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo ushapata wako mwanangu waondoka leo

Nilipokulea mwanangu ulileleka

(Kweli)

Leo umepata wako mwanangu waondoka aeheh

(Kiiitikio)

Mama leo umepata wako

Mwanangu unaondoka leo

Mama kaanze maisha yako

Mwanangu unaondoka aeheh

Mama kawatunze wakwe zako

Mwanangu unaondoka leo

Mama kampende mume wako

Mwanangu unaondoka aeheh

Boga ulilolipenda mwanangu lipende na ua lake

Bwana uliempenda mwanangu mpende na ndugu zake

Lolote likikushinda mwanagu uende kwa wazazi wake

Nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo umepata wako mwanangu unaondoka aeesh

Boga ulilolipenda mwanangu lipende na ua lake

Mtu uliempenda mwanangu mpende na ndugu zake

Lolote likikushinda mwanangu uende kwa wazee wake

(Kiitikio)

Nilipokulea mwanangu ulileleka leo umepata wako

Leo umepata wako mwanangu unaondoka aeesh

Mama leo umapata wako

Mwanangu waondoka aeesh

Dada yaanze maisha yako, mwanangu waondoka aeesh

Mama kampende mume wako

Mwanangu unaondoka aeesh

Dada kampe mapenzi yako, mwanangu unaondoka eesh

Haya yote ni maisha

Mwanangu nawewe kajitahidi

Yasije kubabaisha

Mwanangu kuchekwa huna budi

Mgaie visokwisha mkwe wangu mzidishe mudi

Nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo umepata wako mwanangu unaondoka eesh

Nasema yote ni maisha mwanangu nawe kajitahidi

Yasijekubabaisha mwanangu kuchekwa huna budi

Mgaie visokwisha mkwe wangu mzidishie mdadi

(Kiitikio)

Nilipokulea mwanangu ulileleka

Leo umpata wako mwanangu unaondoka aehe

Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka aehe

Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka aehe

Mama kawapende wakwe zako mwanangu unaondoka aehe

Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka aehe

Kuna videge viwili mwanangu vitakuja na tishio

Vitajileta jileta kwa njia ya matamano

Jua raha ya mapenzi mwanangu kalale na mumeo

Nilipokulea mwanangu ulileleka leo umepata wako mwanangu unaondoka aehe

Nasema kuna ndege wawili mwanangu watakuja na tishio

Watakuwata kufata kwa njia ya matamano

Jua raha ya mapenzi mwanangu ulale na mumeo

(Kiitikio)

Nilipokulea manangu ulileleka

Leo umepata wako mwanangu unaondoka aehe

Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka aehe

Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka aehe

Mama utunze heshima yako mwanangu unaondoka aehe

Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka aehe

Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka aehe

Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka aehe

Nenda salaama ahaa salaama x2

Nenda salaama mwanangu salaama

Nenda salaama ahaa salaama

Tutaonana tena Mungu akipenda

Nenda salaama ahaa salaama

Kwa uwezo wa Allah utadumu naye huyo

Nenda salaama aah salaama x3

Kweupee kule pwani kweupe kuna madege meupe x3

Kweupee kule pwani kweupe kuna madoa meupe x3

Kweupee kule pwani kweupe kuna na njiwa weupe

Kweupee kule pwani kweupe kuna madoa meupe

Nenda salaama aah salaama x2

Nenda salaama mwanangu salaama

Nenda salaama ahaa salaama

(Kiitikio)

Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka aeh

Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka aeh

Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka aeh

Mama utunze heshima yako mwanangu unaondoka aeh

Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka aeh

Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka aeh

Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka aeh

Mama utunze heshima yako mwanangu unaondoka aeh

KIAMBATISHO B: VIBALI VYA UTAFITI


REPUBLIC OF KENYA


**NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **494165** Date of Issue: **13/January/2025**

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Mr. FADHLI HAMISI WENDO of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kwale on the topic: MAUDHUI YA UKUNGWI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARABU for the period ending : 13/January/2026.

License No: **NACOSTI/P/25/415024**

494165
Applicant Identification Number


Director General
**NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY &
INNOVATION**

Verification QR Code



**NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.**

See overleaf for conditions

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)

Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

The National Commission for Science, Technology and Innovation, hereafter referred to as the Commission, was established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
 - i. Endanger national security
 - ii. Adversely affect the lives of Kenyans
 - iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
 - iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
 - v. Adversely affect the environment
 - vi. Adversely affect the rights of communities
 - vii. Endanger public safety and national cohesion
 - viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke